epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Ijumaa Mei 24, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581686
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22

**EDERSON KUONDOKA MAN CITY**

UKURASA WA 3

**MAJALIWA: KUANZIA SASA MAGARI YA WANAFUNZI YAWE NA WALEZI WAWILI**



UKURASA WA 4

**MAKONDA AAGIZA KUKAMATWA FUNDI UMEME ZAHANATI YENYE 'MADUDU'**



UKURASA WA 8

**HELIKOPTA ZA WAGONJWA KUTUA MLOGANZILA**

# Mlipuko ulivyoua 11 kiwanda cha sukari

• **Maongezi** ya simu yanusuru wawili... *Endelea ukurasa 2*



Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Morogoro, SACP Alex Mkama



Sehemu ya chumba cha uendeshaji mitambo 'control room' walipokuwa wamekaa wataalamu waliopoteza maisha wa Kiwanda cha Sukari cha Mtibwa, Turiani wilayani Mvomero, mkoani Morogoro, usiku wa kuamkia jana.
**PICHA: IDDA MUSHI**

## Wadau 1,673 wamchangia Lissu mil 20/- kwa siku tano

UKURASA 2

JANGA UKIMWI

## Tabia bado ni donda sugu

UK.4

**MICHEZO** **UWANJA WA AFCON WATENGEWA BIL.55/-** UK.24 **KATUNI** UK.6



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akimuapisha Kapteni Hussein Mohamed Seif kuwa Naibu Mkuu wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM), Ikulu jijini Zanzibar jana. Katikati ni Katibu Mkuu Kiongozi, Mhandisi Zena Ahmed Said. **PICHA: IKULU**

# Wadau 1,673 wamchangia Lissu mil 20/- kwa siku tano

**Na Jenifer Gilla**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu amesema mchango wa kumnunulia gari umefika Sh. milioni 20 ndani ya siku tano tangu kuanza kwa harambee hiyo.

Kupitia video fupi aliyoiweka jana kwenye ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa X, Lissu alisema ameshapokea Sh. milioni 20 sawa na wastani wa Sh. milioni nne kwa siku.

Alishukuru Watanzania kwa kumchangia kiasi hicho cha fedha na kuwaomba kuendelea kuchangia ili kufikia malengo ya kununua gari jipya ili lile la zamani liwekwe Makumbusho ya Taifa kwa ajili ya vizazi vijavyo kujifunza.

Lissu alieleza kuwa watu waliomchangia fedha hizo mpaka jana wakati anatoa taarifa ni 1,673 sawa na wastani wa Sh. 12,000 kwa kila mchangiaji.

"Ninawaomba kuendelea kuchangia kwa kiasi chochote mlichonacho ili gari lipatikane na kazi ya ukombozi wa wananchi iendelee.

"Elfu moja yako, Sh. 10 yako au kiasi chochote ulichonacho kitatuwezesha kufanya kazi kubwa ya ukombozi wa umma ambao unahitajika," Lissu alisema.

Wiki iliyopita Lissu alikabidhiwa gari lake aina ya Toyota Land Cruizer V8, VXR na Jehi la Polisi mkoani Dodoma ikiwa imepita takriban miaka saba tangu liliposhikiliwa na jeshi hilo baada ya mwanasiasa huyo kushambuliwa kwa kupigwa risasi akiwa kwenye gari hilo na watu wasiojulikana, nyumbani kwake Area D, Septemba 7, 2017.

Baada ya kukabidhiwa gari hiyo, Lissu alisema atalitengeneza ili aendee kulitumia katika shughuli zake za kisiasa mpaka pale litakapochoka, lakini wafuasi wake walisema watamchangia fedha za kununua gari lingine ili hilo liwe ukumbusho juu ya kile kilichomsibu.

Mwanaharakati Maria Sarungi ndiye aliyeanzisha harambee ya kumchangia fedha Lissu ili anunue gari lingine. Kupitia ukurasa wake wa kijamii wa Instagram na X. Maria aliweka tangazo linalosomeka: "Tumchangie Tundu Lissu anunue gari jipya," akiambatanisha namba za kupokea fedha.

Hoja hiyo iliungwa mkono na watu mbalimbali akiwamo aliyekuwa Meya wa Manispaa ya Ubungo, Boniface Jacob aliyeahidi kuchangia Sh. milioni mbili ili kumwezesha kiongozi huyo kununua gari na Godbless Lema aliyeandika ujumbe wa kuhamasisha kwenye ukurasa wake wa mtandao wa X.

# Mlipuko ulivyoua 11 kiwanda cha sukari

**Na Idda Mushi, MVOMERO**

"NDANI ya chumba cha uendeshaji wa mitambo, tulikuwa kama wataalamu 16. Mimi nilitoka nje kuongea na simu, vinginevyo ningekuwa miongoni mwa waliopoteza maisha.

"Pia meneja mkuu wa kiwanda naye alitoka muda huo kwenda kwenye boiler (mtambo wa kuchemshia) kukagua shughuli zinazoendelea kama ziko sawa."

Hiyo ni kauli ya Meneja wa Kitengo cha Umeme na Vifaa wa Kiwanda cha Sukari cha Mtibwa, Juma Palamba, alipozungumza na mwandishi wa Habari hii akielezea tukio la mlipuko uliotokea katika chumba maalum cha uendeshaji wa mitambo na kusababisha vifo vya watu 11 na mmoja kujeruhiwa.

Waliofariki dunia katika tukio hilo ni raia watatu wa kigeni kutoka Brazil, Kenya na India na Watanzania wawili ambao walijeruhiwa wakati wakifanya majaribio ya mtambo wa mvuke uliokuwa umeboreshwa kwa kuongezewa nguvu ya uendeshaji.

Alisema tukio hilo lilitokea Mei 23, mwaka huu, katika kiwanda hicho kilichoko Turiani, Mvomero mkoani Morogoro.

Palamba alisema akiwa anaongea na simu, alimwona msaidizi wake mwingine akiwa nje pia anaongea na simu na kwamba wao na wenzao ambao ni meneja uzalishaji ambaye alikuwa akikaimu nafasi ya meneja wa kiwanda walinusurika.

Waliojeruhiwa katika tukio hilo, ni opereta na msaidizi wake ambao walikuwa ndani lakini inaonekana mvuke haukuwapiga moja kwa moja kama wengine waliofariki dunia.

Mwandishi wa habari hii alifika jana alfajiri kiwandani hapo baada ya kupata taarifa za tukio na kushuhudia eneo la ajali huku miili ikiwa imeondolewa kupelekwa kuhifadhiwa hospitalini.

Palamba alisema hitilafu hiyo imetokea wakati wa majaribio ya mitambo iliyoongezwa uwezo na walikuwa katika hatua ya mwisho ya majaribio ili leo kuanza rasmi msimu mpya wa uzalishaji.

"Ni ajali ambayo imetokea baada ya 'pipe' (bomba) ambayo inapokea 'steam' (mvuke) kupeleka kwenye mtambo wa kuchemshia inayotoa fito 45 na kipimo cha nyuzi joto inafikia hadi 450.

"Tukio lilivyotokea ni kwamba walishazalisha mvuke, wakaufungulia kuupeleka eneo la kuzalisha umeme. Lengo kubwa lilikuwa kufanya majaribio baada ya kuongezea nguvu injini ya mvuke, maji na gesi yetu ambayo mwanzo ilikuwa ikitumia mvuke wa fiyo (bar) 24 na nyuzi joto 300," alisema.

Pia alisema katika kuboresha mifumo huwa kuna mabadiliko mbalimbali yanafanyika kabla ya kuwezesha mtambo wa kuchemshia kuhimili kupokea na kutoa mvuke kwa kiwango kikubwa zaidi sambamba na kupima kama injini itahimili mabadiliko husika ndiyo maana jaribio la kwanza lilikuwa kuiongezea nguvu njia iwe na uwezo wa kupokea 'bar' 45.

Alisema jaribio la pili lilikuwa la kubadilisha mabomba ya kusafirishia mvuke kwa sababu kuna sehemu ambazo mabomba yalikuwa na uwezo wa kupokea fito 24 tu, hivyo kazi ya kubadilisha ilifanyika.

"Leo (jana) sasa baada ya kufanya majaribio ili kesho (leo) tuanze uzalishaji rasmi, ndipo hiyo hitilafu ikatokea. Bahati mbaya sasa mvuke ulipokewa kabla ya kufikia kuzungusha mtambo wa mvuke.

"Wakati tukisubiri mvuke na nyuzi joto vipande ili kuruhusu mtambo kuwashwa, wakagundua katika hayo mabomba yaliyobadilishwa ambayo pia yana maeneo ya maungio yanayoruhusu kutanuka na kusinyaa, baada ya kupokea bar 45, pakaonekana sehemu moja ni dhaifu na pakachanika, hivyo kusababisha mvuke wote uliokuwa ukitokea eneo la kuchemshia kutoka nje," alisema.

Alisema mvuke huo wote uliokuwa ukisafirishwa kwa mwendokasi wa kati ya 30 hadi 45 kwa nyuzi joto 450, wote ulikwenda kwenye chumba cha kuendesha mitambo ambako waendesha mitambo, yaani maopereta na wataalam wengine, akiwemo mtengenezaji wa mtambo wa mvuke, wataalamu wa kutoka vitengo mbalimbali na wasaidizi wao wote walikuwa wakiangalia majaribio, ili kila mmoja aifanyie kazi eneo lake.

Kwa mujibu wa mtaalam huyo, miongoni mwa watu 11 waliofariki dunia ni pamoja na mtengenezaji na mwendeshaji wa mtambo huo wa mvuke raia wa Brazil, mhandisi mwingine raia wa Kenya ambaye ni msaidizi wake katika kitengo cha umeme, mhandisi mwingine raia wa India na wataalamu wanane, raia wa Tanzania.

**KAMANDA ATHIBITISHA**

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Kamishna Mwandamizi wa Polisi (SACP) Alex Mkama, aliyefika eneo la tukio, alisema hitilafu hiyo ya umeme ilitokea kwenye mtambo wa kupitisha mvuke wa kuzalisha umeme kiwandani hapo.

Mkama alisema majeruhi wawili wa ajali hiyo, akiwamo Mtanzania mmoja na raia mwingine wa kigeni (majina bado) wamepelekwa Hospitali ya Misheni ya Bwagala kwa matibabu zaidi

**TANESCO, ZIMAMOTO**

Kamanda wa Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Morogoro Shaban Marugujo, alisema: "Kilichotokea ni bomba la mvuke kutoka boiler namba 4 kwenda chumba cha kuzalisha umeme lenye uwezo wa kubeba bar 45 kwenye maungio yake lilishindwa kuhimili, hivyo kuachia na kwenda kupiga kwenye chumba cha mawasiliano walikuwako watu na kufariki dunia papo hapo."

Alisema hadi sasa chanzo cha ajali hiyo hakijafahamika na uchunguzi zaidi wa tukio hilo bado unaendelea kwa kushirikisha wataalam mbalimbali.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Turiani, Dk. David Ruchwanisa, alisema usiku wa kuamkia Mei 23, majira ya saa 10:00 usiku walipokea majeruhi wawili wa jinsia ya kiume na waliwapatia matibabu na baadaye kupewa rufani kwenda Hospitali ya Benjamini Mkapa, Dodoma kwa matibabu zaidi kutokana na hali zao kuwa mbaya.

Alisema majeruhi hao wameungua maeneo mbalimbali ya miili yao ikiwemo tumboni, kifuani miguuni na mikononi.

Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mkoa wa Morogoro Mhandisi Fadhili Chilombe, alisema mfumo huo ulikuwa unatumia umeme kidogo wakati wa kuwasha na badaye kujiendesha wenyewe.

Alisema kutokana na mlipuko huo kwa sasa hautaweza kujiendesha na kwamba pale watakapohitaji huduma ya umeme, TANESCO wako tayari kuwahudumia ili shughuli za kiwanda zisisimame.

# Mabasi ya wanafunzi kuwa na walezi wawili

**Na Paul Mabeja,** DODOMA



WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa (pichani), ameelekeza mabasi yote ya shule yanayotumika kupeleka shuleni na kuwarudisha nyumbani wanafunzi lazima yawe na walezi wawili wa kike na wa kiume kila moja.

Pia amewataka wazazi na walezi kufuatilia mwenendo wa watoto wanapokwenda shuleni, mahudhurio na namna wanavyotekeleza kazi za masomo wanazopewa na walimu.

Kadhalika, amesema serikali inaendelea kuimarisha mahudhurio ya watoto shuleni kwa kuzungumza na wazazi ili kuhakikisha kila mzazi anasimamia mahudhurio ya mtoto wake shuleni anapofika shuleni na kuingia darasani, lakini anaporudi nyumbani mzazi anafuatiliaje mwenendo wa mtoto wake kujiridhisha kama alikwenda shuleni.

Majaliwa alisema hayo jana bungeni jijini hapa wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Nancy Nyalusi, aliyehoji kama serikali haioni haja ya kutunga sheria ili kulinda usalama wa wanafunzi wanapokuwa kwenye magari.

Katika swali lake, Nyalusi alisema ukuaji wa sekta ya elimu na ongezeko la shule binafsi vimesababisha kuongezeka kwa huduma ya usafiri kwa wanafunzi kupitia mabasi maalum jambo ambalo lina athari nyingi.

“Je, serikali haioni haja ya kutunga sheria inayolinda usalama kwa magari yote yanayosafirisha wanafunzi?” alihoji mbunge huyo.

Akijibu swali hilo, Waziri Mkuu alisema ziko sheria za vyombo vya usalama vyote vinavyotumia moto yakiwamo mabasi yanayobeba wanafunzi.

“Sheria hizi zinatakiwa kufuatwa kwa ajili ya usalama wa abiria, wakiwamo watoto wetu, lakini kwenye eneo la mabasi ya wanafunzi tumeongeza kanuni ambazo zinawabana wamiliki wa shule kuimarisha mabasi yao na kutambulika,” alisema.

Alisema miongoni mwa kanuni hizo ni lazima dereva awe na sifa ya kuendesha mabasi ya abiria na kubeba wanafunzi, lazime yapakwe rangi ya njano ili popote yanapopita yajulikane ni ya shule na yawe na maandishi makubwa ubavuni na mbele.

”Tumeanza kuona utekelezaji huo unafanyika lakini bado tunajua tuna shule zina watoto wa kike na wa kiume. kila inapofanya safari basi ya kwenda kuwafuata wanafunzi na kuwapeleka shuleni ni lazima liwe na walezi wawili wa kiume na kike kwa ajili ya usalama wa watoto wetu inapotokea dharura wapate huduma kulingana na jinsia.

Alisema hata wanapowapeleka likizo ni lazima wasindikizwe kwa wazazi wao kwahiyo eneo hili tumeweza kulisimamia, kazi kubwa ambayo tunafanya sasa ni kufanya mapitio kwa kuwa na vikao vya pamoja kati ya wizara ya elimu na TAMISEMI na wadau waliowekeza kwenye sekta ya elimu.

Alisisitiza kuwa serikali imetoa fursa kwa watanzania kuwekeza kwenye sekta ya elimu na mafanikio makubwa yamepatikana ambapo kuna shule za awali, msingi, sekondari na sekta binafsi nyingi.

“Tunaendelea kufuatilia masharti yote ambayo tumeweka kwenye vyombo hivi vya usafiri kwa ajili ya usalama wa watoto wetu, kwa sheria zote zinazosimamia vyombo vya moto kwa ajili ya usalama wa abiria wanaotumia mabasi haya,”amesisitiza.

Mwaka jana, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitoa waraka unaoelekeza mabasi ya shule kuwa na walezi wawili ikiwa ni moja ya hatua za kukabiliana na matukio ya ukatili dhidi ya watoto yanayofanywa na baadhi ya madereva wa mabasi ya shule na wasaidizi wao, wakiwamo walezi wa watoto hao.

Naye Mbunge wa Sikonge (CCM), Joseph Kakunda, alihoji mkakati wa serikali katika kuhakikisha wanafunzi wanaoanza masomo wanamaliza wote isipokuwa kwa wanaofariki dunia.

Akijibu swali hilo, Waziri Mkuu Majaliwa alisema: “Tunaimarisha ujenzi wa mabweni na hosteli kwaajili ya wanafunzi wa kike na wa kiume ili wasome palepale, walale pale, wacheze pale, lakini pia usimamizi wa maadili yao uweze kuimarika.”

Wakati huohuo, Waziri Mkuu ametumia fursa hiyo kumpongeza Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha kuwa wanafunzi walioacha masomo kwa sababu mbalimbali wanarejeshwa shuleni ili waweze kutimiza ndoto zao.

“Ninampongeza Rais Dk. Samia katika kipindi chake cha uongozi alielekeza wanafunzi wa kike waliochishwa masomo warudi shuleni ili waweze kutimiza ndoto zao.”


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza ‘‘subscribe’’
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona ‘‘E-Paper’’ utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

JANGA UKIMWI

# Tabia bado ni donda sugu

**Na Romana Mallya**

WADAU wa sekta ya afya wameshauri serikali kuweka mazingira rafiki kwa vijana katika vituo vya afya kukabiliana na janga la maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU).

Ni baada ya ripoti mpya ya Shirika la Afya Duniani (WHO) iliyotolewa juzi kuonesha bado kuna kiwango kikubwa cha watu wanaoambukizwa VVU, homa ya ini na magonjwa ya zinaa.

Wakitoa maoni yao kuhusu ripoti hiyo inayoonesha zaidi ya watu milioni moja wa umri wa kuanzia miaka 15 hadi 49 wanaambukizwa kaswende na kisonono kila mwaka, wadau hao walisema jana kuwa wanataka kundi hilo liwekewe mazingira rafiki kwa kuwa ndilo lenye shida.

Akizungumza na Nipashe jana juu ya ripoti hiyo ya WHO, mdau wa masuala ya afya kwa vijana, Catherine Madebe, alisema kwa upande wa Tanzania, changamoto wanayokutana nayo ni rika la vijana wa umri wa kuanzia miaka 15 hadi 24, hawaendi hospitalini kupima kama wana maambukizi.

Alisema wanapoona dalili hukimbilia katika maduka ya dawa kununua dawa na si kupima kujua wana maambukizi ya aina gani.

Catherine alitaja changamoto nyingine ni vijana kutumia kwa kiwango kikubwa dawa za antibaiotiki ambapo hadi afike hospitalini anakuwa tayari na usugu wa dawa.

Alisema hali ya uelewa sahihi wa matumizi ya kondomu kwao ni asilimia 40 licha ya kujua umuhimu wake. Kuna changamoto kwenye kutumia kinga hizo dhidi ya maambukizi ya VVU.

Kutokana na changamoto hizo, Catherine alisema ushirikishwaji wa pamoja kati ya wadau na serikali ni jambo muhimu, hivyo uongezwe.

Alisema serikali inapaswa kutoa elimu juu ya VVU/UKIMWI kwa kuzingatia rika tofauti, hasa kwa vijana, ili wanapoona taarifa husika wapate ujumbe moja kwa moja.

Alisema kuwa mazingira ya hospitalini si rafiki kwa vijana kuzungumza masuala ya afya kuanzia kujikinga.

Mdau huyo alisema wamepiga kelele juu ya suala hilo na sasa kuna baadhi ya vituo vimeweka huduma hizo ingawa si vingi, na kutaka kasi iongezwe ili vijana wapate mahali sahihi pa kwenda.

“Tufanye hivyo ili tuwaambie vijana kuwa sasa hivi tumeshawawekea mazingira rafiki, hivyo ukiwa na changamoto ya kiafya usikimbilie katika duka la dawa na kuchukua dawa na kutengeneza usugu, waende moja kwa moja hospitalini au katika vituo vya afya,” alisema.



Abiria wakisubiri mabasi katika Kituo cha kisasa cha Mwenge, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam mapema wiki hii, licha ya huduma za usafiri kuonekana kusuasua kutokana na mabasi machache yanayoingia kituoni hapo. **PICHA: JOHN BADI**

# Makonda aagiza kukamatwa fundi

**Na Beatrice Shayo,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, amekutana na madudu katika zahanati ya kijiji cha Lemereta, wilayani Longido iliyofungiwa umeme wa njia moja, hivyo kusababisha kushindwa kupima kipimo cha wingi wa damu kwa wajawazito.

Kutokana na madudu hayo, Makonda ameagiza waliosababisha jambo hilo kukamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria na kinidhamu.

Makonda aliibua madudu hayo jana alipofanya ziara ya kukagua miradi katika wilaya ya Longido na kuhoji ni kwa nini zahanati imefungiwa umeme mdogo na kushindwa kufanya baadhi ya vipimo.

Awali, Ofisa Muuguzi wa Zahanati ya Leremeta, Samson Philip, alimweleza Makonda kuwa umeme uliofungwa katika zahanati hiyo ni mdogo, hivyo kusababisha kushindwa kufanya baadhi ya vipimo, vikiwamo wingi wa damu (HB) na shinikizo la damu (BP). Alisema wataka kufanya kipimo cha BP, inawalazimu kuweka betri.

“Lakini mashine ya wingi wa damu huwezi kuweka betri. Inahitaji umeme, hivyo mjamzito akihitaji kufanyiwa kipimo hicho hatuwezi. Tunamwambia aende katika zahanati nyingine,” alisema.

“Mashine zinazohitaji kutumia umeme ni nyingi lakini hatuwezi kuzitumia. Kuna vifaa vinatakiwa kuchemshwa. Hii mashine ipo lakini hatuwezi kuitumia kutokana na huu umeme uliowekwa hapa, hata simu haichaji katika huu umeme, unaweka kuanzia asubuhi hadi jioni iko asilimia 10 tu,” alisema.

Philip alisema wanafanya kazi katika mazingira magumu inamlazimu baadhi ya vifaa aende kuvichemsha katika jiko lake nyumbani kutokana na shida hiyo ya umeme uliofungwa.

Pia alisema hata nyumba wanayoishi, iliyojengwa kwa thamani ya Sh. milioni 90 haina umeme tangu ilivyokamilika Desemba 4, mwaka jana.

Makonda alimtaka Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Wilaya ya Longido, Lazaro Lenoi, kueleza kwa nini walifunga umeme mdogo katika zahanati hiyo na kusababisha wananchi kukosa baadhi ya huduma.

Katika maelezo yake, Lenoi alisema malalamiko hayo ndiyo kwanza ameyasikia tangu umeme ulipofungwa kwenye zahanati hiyo na tayari alishauri uongozi kuwa umeme unaowafaa ni wa njia tatu badala ya ule waliolipia wa njia moja wa Sh 27,000.

Makonda alimhoji Mwenyekiti wa Kijiji, Supuk Melita, kama ni kweli walipewa ushauri na Lenoi wa kuweka umeme wa njia tatu badala ya njia moja na kukiri ni kweli ingawa hawakuwa na uelewa na mtumishi mwingine wa TANESCO aliwajulisha tatizo si njia moja ni ‘main switch’ hali iliyomlazimu kwenda kununua kifaa hicho.

## Majaliwa ataka hatua matumizi mabaya madaraka

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameitaka taasisi zinazoshughulikia hakijinai kuchukua hatua dhidi ya watu ambao wamekuwa wakitumia madaraka kunyang'anya wananchi wanyonge maeneo yao.

Pia amesema kuachwa kwa jinai hiyo kuendelea ni kukuza migogoro ambayo inajihusisha na uvamizi wa ardhi katika maeneo nchini.

Maagizo hayo aliyatoa jana jijini hapa, kupitia hotuba yake iliyosomwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, wakati wa uzinduzi wa kliniki ya ardhi kwenye maonyesho yaliyoandaliwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi katika viwanja vya Bunge.

Aidha, alizikumbusha taasisi zinazoshughulikia jinai kuendelea kuchukua hatua dhidi ya uvamizi wa ardhi kama jinai nyingine hivyo zishughulikiwe haraka.

“Maelekezo haya yanatokana na ukweli kwamba wako baadhi ya wananchi wanakiuka sheria hizi kwa makusudi kwa kuvamia maeneo yenye miliki halali. Tena wakati mwingine maeneo hayo yana miliki za watu wanyonge na kutumia madaraka na nguvu walizonazo kupora miliki za watu wengine.

“Wakati mwingine maeneo yenye umiliki halali wa taasisi za umma pia yamekuwa yakiporwa na baadhi ya watu na kutumiwa kinyume cha sheria na taratibu za nchi,” alisema

Pia alisisitia kuachiwa kwa jinai hiyo kuendelea ni kukuza migogoro ambayo inajihusisha na uvamizi wa ardhi katika maeneo mengi nchini.

Kadhalika, aliagiza taasisi mbalimbali zinazodaiwa kodi ya ardhi na malimbikizo kulipa mapema kabla ya muda wa mmoja tangu Mei Mosi hadi 31, mwaka huu, uliowekwa wa kulipa kodi na malimbikizo hayo haujaisha.

“Waziri Mkuu amesikia ukiwatangazia wadaiwa wote kulipa kodi ya pango la ardhi na umetoa muda wa mwezi mmoja kuanzia Mei Mosi, anakuhakikishia kuwa kupitia serikali tutaunga mkono jambo hili kwa nguvu zote ili tupate mafanikio makubwa,” alisema.

Alizisisitiza taasisi zote ambazo zinamiliki ardhi ziendelee kuwasiliana na Wizara ya Ardhi ili kuwa na uhakika wa hali halisi ya umiliki wa ardhi hizo kwa sasa na endapo kuna uvamizi uliokwisha kufanyika hatua zichukuliwe kwa haraka.

Pia aliwasisitiza wabunge kuisaidia serikali, wizara kuwa mstari wa mbele kwa kutoa taarifa ya ukiukwaji wa sheria za ardhi katika maeneo mbalimbali nchini pamoja na kutoa elimu kwa wananchi wote katika maeneo yao hasa kuwaasa kuacha tabia ya uvamizi katika maeneo yaliyopangwa kihalali na kumilikishwa kihalali kwa watu wengine.

# Serikali yatangazia kiama wavuvi haramu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeagiza wananchi na wavuvi wote nchini kupiga vita uvuvi haramu ili rasilimali za uvuvi ziwe endelevu kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Alexander Mnyeti (pichani), alisema hayo jana bungeni jijini hapa, wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Furaha Matondo. Alitaka kujua lini serikali itavipatia mafunzo vikundi vya usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi ili kukabiliana na uvuvi haramu.



Akijibu swali hilo, Mnyeti alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeendelea kutoa mafunzo kwa vikundi hivyo kulingana na upatikanaji wa rasilimali fedha.

Alisema katika mwaka 2023/24, wizara kwa kushirikiana na shirika lisilo la kiserikali la Tanzania Nature Conservancy (TNC) ilitoa mafunzo juu ya usimamizi wa rasilimali na athari za uvuvi haramu kwa wanachama 558 wa BMUs.

Wanachama hao na idadi kwenye mabano ni kutoka vijiji vya Karungu (62), Mandakerenge (62) Mtakuja (62) Manda Uhuru (62), Mkinga (62), Ntanganyika (62), Isasa (62), Kichangani (62) na Kipili (62) katika Ziwa Tanganyika.

Pia alisema wizara imeendelea kutoa mafunzo juu ya athari za uvuvi haramu kwa viongozi 144 wa vikundi vinane na idadi yao kwenye mabano Dunda (18), Kaole (18) Mlingotini (18), Kitame (18), Changuahela (18) ,Pande (18), Kisutu (18) na Kondo (18) katika Halmashauri ya Bagamoyo na Viongozi 108 wa BMU sita za Maloo (18), Mchinga I (18) Mchinga II (18), Kijiweni (18), Mvuleni Mashariki (18) na Ruvu (18) katika Halmashauri ya Lindi Mjini.

"Mheshimwa Spika, wizara inatoa wito kwa wananchi na wavuvi wote hapa nchini kupiga vita uvuvi haramu ili rasilimali za uvuvi ziweze kuwa endelevu kwa ajili ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo," alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila (katikati), Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Beng'I Issa (wa pili kushoto), Mshauri wa Rais wa Mambo ya Wanawake na Makundi Maalum, Sophia Mjema (wa pili kulia), Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo (kushoto) na Mshauri wa Uchumi wa Mkoa huo, Dk. Elizabeth Mshote, wakifuatilia jambo wakati wa uzinduzi wa programu ya Imarisha Uchumi na Mama Samia (IMASA), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbaroni kwa madai ya wizi wa magari

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limekamata watu wanne na magari 12 yanayodaiwa kuibwa na kufutwa namba za usajili kisha kuuzwa.

Kamanda wa Polisi wa Kanda hiyo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumzia operesheni maalum iliyofanyika kuanzia Desemba, 2023 hadi Mei 22, mwaka huu.

Alisema operesheni hiyo ilihusisha kamisheni mbalimbali za polisi ikiwamo ile ya kisayansi na kuwezesha kupatikana kwa magari 12 na bajaji tano za wizi ambavyo tayari vimetambuliwa na wamiliki.

"Katika operesheni hii, amekamatwa Haruni Selemani, maarufu kwa jina la Haruni (34), mkazi wa Yombo Makangarawe, wilayani Temeke na wenzake watatu," alisema.

Kamanda Muliro alisema watuhumiwa hao wanadaiwa walikuwa wakiiba magari hayo, kufuta namba za usajili wa gari (Chesis) na kubadilisha namba za usajili halafu kuyauza tena yakiwa na kadi za bandia.

Katika hatua nyingine, alisema polisi wamewakamata watuhumiwa watatu akiwamo, Ezekiel Amani (30), maarufu kama Makundi, mkazi wa Buza Kanisani na wenzake wawili kwa tuhuma za kuhujumu miundombinu ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Alisema watuhumiwa hao walikamatwa Mei 15, mwaka huu, eneo la Kisarawe II, Kigamboni wakiwa wanaiba nyaya za umeme zilizokuwa juu kwenye nguzo.

Kamanda Muliro alisema watuhumiwa hao wanadaiwa kukamatwa na waya wa umeme wenye urefu wa mita 572 wa milimita 50 waliokuwa tayari wamekwishaukata, glovu za kushikia nyanya za TANESCO jozi moja, mkanda wa kupandia kwenye nguzo na kifaa cha kukata umeme inapotokea hitilafu.

Kamanda Muliro alisema watuhumiwa hao walitarajia kuwafikisha mahakamani jana kwa tuhuma hizo

"Tunawaomba wananchi kuendelea kutoa taarifa za wahalifu na hatutakuwa na huruma, kwani tutawashughulikia vikali kwa mifumo ya kisheria, ikiwa ni pamoja na kuwafikisha mahakamani," alisema Muliro.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
20.05.2024

## TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **26.05.2024** hadi **02.06.2024** kampuni ya **CEVA Interfreight** itasafirisha mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka Bandari ya **Dar es salaam** kuelekea **Mzenga** , gari hilo lenye namba za usajili

   **NRB97300 / NRB54202**
   **DSOOTG GP / NRB53910**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 28.0  Upana - mita 5.50  Kimo - mita 4.60**

3. Njia itakayotumika: Bandari ya **Dar Es Salaam** hadi **Mzenga** kupitia Barabara ya **Morogoro**, gari litasafiri muda wa mchana **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni).**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**



**TANGAZO LA MKUTANO MKUU WA MWISHO WA WANAHISA WA KAMPUNI YA**
**MITCHELL DRILLING TANZANIA LIMITED**
**Cheti cha Usajili No. 97193**
Sheria ya Makampuni, 2002 (Kifungu 334 (1))

Umma na wahusika wanafahamishwa kutakua na mkutano mkuu wa mwisho wa wanahisa wa kampuni la Mitchell Drilling Tanzania Limited, yenye usajili namba 97193 kitakachofanyika tarehe **24 Juni 2024** ofisini kwa mfilisi saa 4:00 asubuhi ambapo mfilisi atatoa hesabu ya kufungwa kwa hiari kwa kampuni.

Mfilisi: **JOSEPH LYIMO**
Amwani ya Mfilisi: **PricewaterhouseCoopers Limited, Pemba House, 369 Toure Drive, Oyster Bay. P.O. Box 45. Dar es Salaam. Tanzania**

Tarehe ya kuchaguliwa: 20 DESEMBA 2023
Amechaguliwa na: **WAMILIKI WA KAMPUNI**

**Sahihi** ......................................... **Tarehe:** 20 MEI 2024

**Jina: JOSEPH LYIMO**

**Imetolewa na;**
**JOSEPH LYIMO**
**MITCHELL DRILLING TANZANIA LIMITED**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kinamama nchini sasa wahamasishwe matumizi nishati safi

**MATUMIZI** ya jikoni kwa asilimia kubwa kwa kinamama wa vijijini ni nishati ya kuni na mkaa ambayo huchangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa hali ya hewa.

Moshi wanaovuta kutoka kwenye kuni na mkaa husababisha athari kubwa kwa magonjwa yanayosababishwa na hewa chafu.

Hivyo ulinzi wa afya ya mama, familia, mazingira na taifa dhidi ya mabadiliko ya tabianchi ni lazima uanzie jikoni.

Rais Samia Suluhu Hassan, amekuwa kinara wa kutangaza matumizi ya nishati safi ya kupikia na lazima taifa lianze sasa kubadilisha nishati inayotumiwa kupikia.

Mara kwa mara anapokuwa kwenye majukwaa mbalimbali ya matumizi ya nishati safi ya kupikia, Rais anasema huwezi kumaliza au kupunguza ukataji miti unaoangamiza misitu kama hutaligusa jiko.

Kampeni ya Rais imefanya mengi, Watanzania wameelezwa umuhimu wa matumizi ya teknolojia za kupikia zinazopunguza madhara kiafya, athari kwa mazingira na kijamii.

Na sasa Rais amelifikisha taifa kwenye kutekeleza Mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia 2024 - 2034.

Analenga kaya zenye 'jiko safi na salama', ambayo asilimia 80 ya Watanzania watakuwa wanatumia jiko lenye nishati safi ya kupikia ifikapo 2034.

Pamoja na kuwaondoa kinamama katika matumizi ya kuni na mkaa na kutumia nishati safi, pia taasisi kubwa ambazo zinahudumia watu wengi kupata chakula, zinahimizwa kuhama kwenye matumizi ya kuni na mkaa na kuhamia kwenye nishati safi ili kupunguza uharibifu wa hewa na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Hata hivyo, ili kufanikiwa katika matumizi ya nishati safi ipo haja ya kuwa uhamasishaji wa kutumia majiko yanayotumia nishati safi na yapatikane kwa urahisi ili wanayoyahitaji wasipate vikwazo kwa kuyapata.

Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS) inaeleza kuwa Tanzania Bara ina takribani kaya milioni 13.9.

Kufikia azma hiyo kaya zenye 'jiko safi na wakuu wa mikoa na wilaya wasimamie matumizi ya nishati safi ya kupikia na pia wizara na taasisi za umma kadhalika na sekta binafsi kuzingatia matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kulinda mazingira na kuepusha athari nyingi zinazotokana na kutumia nishati zisizo safi.

Mwaka jana Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira iliagiza taasisi zote zinazohudumia watu zaidi ya 100, ifikapo Januari, mwaka huu, ziache kutumia kuni na mkaa kupikia.


Ofisi ya Makamu wa Rais, katika mikakati yake inaeleza kuwa hilo limefanyika na taasisi nyingi zikiwamo za umma kuanzia Magereza, kambi za jeshi, shule za sekondari, vyuo vya ualimu na vikuu vimeanza kutumia nishati safi ya kupikia.

Pia, juhudi zinafanywa na kila taasisi inayohusika na nishati na katika mbio za Mwenge wa Uhuru, mwaka huu, ujumbe mkubwa unaobebwa ni uhamasishaji wa matumizi ya nishati safi kupikia.

Uhamasishaji huo utasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza matumizi ya kuni na mkaa na kuepusha athari zinazosababishwa na hewa chafu inayotokana na kuvuta moshi mchafu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Uchumi unavyoweza 'kutendwa' kwa 'Kilimo Kwanza' akafikiwa Mtanzania

Na Tuntule Swebe

**SI** mahali pa mjadala, kilimo kinahitajika na kina manufaa kila kona duniani, ikiwamo nchini. Nafurahi hadi sasa tuna baadhi ya mazao ya kimkakati yanaendelezwa kulinda uchumi na lishe yetu.

Hapo nami nasisitiza kwamba bidii na udhibiti chanya ufanyike, ikiwamo matumizi sahihi ya maji shambani. Ili sekta hiyo kuimarika, serikali inaweza kuianzishia katika namna bora zaidi, suala la udhibiti wa huduma za maji,

Hapo ndipo pataanza ushuhuda wa kuimarika uzalishaji mazao mengi ya biashara na chakula ustawi wa sekta mifugo na uzalishaji samaki. Kwa ujumla, tunaona namna ukuzaji kilimo mseto unachukua nafasi, kukawapo ongezeko la pato kwa sekta kilimo, mifugo na mazao ya baharini.

Sera ya Kilimo nchini iliyofanyiwa kazi mwaka 2013, inaangaza maendeleo endelevu ya sekta hiyo, kwa manufaa ya kiuchumi, kijamii na kimazingira kwa wananchi wake.

Serikali inatazamia kuendeleza usimamizi wa udhibiti wa maji, kuhimiza uimarishaji wa mazao mengi na kuongeza uzalishaji wa mifugo na samaki.

Hali kadhalika, kuna angalizo la ukuzaji kilimo mseto na kuelekeza mazao thamani ya juu, pia chakula cha kutosha, vikwazo vya uzalishaji kitaifa vikaondolewa.

Ni hatua inayoendana na urekebishaji, pia kuboresha usafi, kupunguza magonjwa ya kuambukiza na kuhimili vyanzo mbalimbali vya shughuli za kuongeza kipato, kwa ajili ya kuongeza mapato ya wakulima wadogo.

Hilo ni ongezeko na ukuaji endelevu wa uzalishaji wa kilimo unaotokana na mabadiliko ya kimuundo, yanayolenga kuongeza tija, kuendeleza teknolojia mpya na kuzalisha bidhaa mpya.

Kwa ajili hiyo, mikakati ifuatayo ya maendeleo itatumika kama ilivyopangwa: Kuimarishwa usimamizi wa utafiti wa kilimo, ugani na mafunzo; ufuatiliaji na tathmini ya karibu ya maendeleo ya kilimo; utambulisho wa bidhaa mpya, teknolojia.

Mengine yanatajwa ni kukuzwa michakato ya ushiriki wa sekta binafsi katika biashara za kilimo; mapitio ya kila mara ya athari za sera za kilimo; kudhibiti ubora wa pembejeo na bidhaa za kilimo; hata wa wadudu na magonjwa husika.

Kuna eneo lililotajwa la utoaji mfumo wa kutosha wa kisheria na udhibiti; ukuzaji na ufuatiliaji wa vyama vya wakulima na katika kuboresha usimamizi wa maliasili una hatua zake, pia.

Vilevile, kuna ukuzaji miundo ya kitaasisi katika sekta ya kilimo; kukuza umwagiliaji mdogo; miundo ya usimamizi wa sera ili kueleza vipaumbele vya sekta na kutafsiri uamuzi mkubwa kisera katika hatua mahsusi za sekta na kufuatilia athari za mageuzi ya sera kwenye kilimo.

Mkakati pia naamini itachangia maendeleo ya mifumo jumuishi zaidi ya kilimo na chakula, ili kupunguza umaskini kiserikali, itakuza uwekezaji wa sekta kilimo, tija kubwa ya kilimo miongoni mwa wakulima maskini, na shughuli za kuzalisha mapato nje ya mashamba.

Kwa maana hiyo, mikakati ya sera italenga kuimarisha uzalishaji kilimo kupitia teknolojia iliyoboreshwa, kuhimiza uwekezaji zaidi katika mifumo ya umwagiliaji ya wakulima wadogo, na kuanzisha ukuzaji miradi ya kupunguza umaskini itakayotekelezwa na asasi za kijamii na kiraia.

Inatajwa haja ya kukuzwa usawa kijinsia katika maendeleo ya kilimo, ili kuhakikisha wanawake wanadhibiti rasilimali za uzalishaji mali, zikiwamo ardhi na maji,

Muhimu ni juhudi zitazingatia kuendeleza programu za kuhamasisha umma kuhusu masuala ya kijinsia, na kutunga sheria zinazohimiza usawa wa kijinsia katika umiliki na udhibiti wa rasilimali za uzalishaji na kuhimiza tasisi zisizo za kiserikali na mashirika ya kijamii kuanzisha programu na miradi inayowasaidia wakulima wanawake.

Kuhusu utawala, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mazingira na Ushirika ndiyo taasisi yenye dhamana ya utekelezaji na uratibu wa mikakati.

Hapo, baadhi ya viashiria vya utendaji vitakavyotumika vinatajwa kuwa uhusiano wa pato la taifa na ukuaji wa sekta kilimo kwa ujumla.

Kimkoa, kunatajwa Maendeleo ya Kilimo na Vijijini; Mifugo; Mazingira; Chakula na Lishe; Uvuvi; Ardhi na udongo; na Maji, mzuzi ukitoka kwa Rais wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete na itakadi 'Kilimo Kwanza.'

# Wataka sauti zote kusikika kuelekea uchaguzi ujao

**Na Elizabeth Zaya**

TAASISI ya Foundation for Civil Society (FCS), imesema kuwa kuna haja ya kila sauti kwenye jamii kupewa nafasi ya kusikika ili kufikia ustawi wa taifa hasa tunapoelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu.

Kadhalika, amesema wametambua hatua ambayo imefanywa na serikali katika nafasi muhimu ya michakato ya kidemokrasia katika kuunda mustakabali wa taifa na kwamba maandamano ya amani ya hivi karibuni yanasisitiza hitaji la mabadiliko na ushirikishwaji wa raia katika kukuza sauti ya pamoja na kuongeza ufanisi wa kisiasa.

Hayo yamesemwa na Mshauri wa Mikakati ya Taasisi ya Foundation for Civil Society (FCS), Prudence Glorious, wakati wa uzinduzi wa maandalizi ya kuelekea kwenye Wiki ya Asasi za Kiraia (AZAKi) ambayo inafanyika kwa mara ya sita.

"Hii inaalika kila Mtanzania, kuanzia wanaharakati wa ngazi za chini hadi viongozi wa kitaifa wa biashara, kuchangia maarifa na uzoefu wao, muhimu, inahusu kuhakikisha kwamba sauti ya kila mtu inasikika katika mazungumzo ambayo yanaunda mustakabali wa taifa letu, hasa katika kuelekea uchaguzi," alisema Prudence.

"Wakati Watanzania wakijiandaa kushiriki katika chaguzi muhimu, tukio hili linatambua nafasi muhimu ya michakato ya kidemokrasia katika kuunda mustakabali wa taifa."

Kadhalika, alisema mwaka huu wiki hiyo itafanyika kitofauti kwa mijadala yake kufanyika kwa mitindo ya kuketi kwenye mikeka, vigoda na vijiweni, ili kufikisha ujumbe kwa urahisi kwa wananchi.

Alisema wiki hiyo itafanyika Septemba 9 hadi 13 mkoani Arusha na inatarajia kuwa na washiriki zaidi ya 500 ambayo wataketi kujadili katika mikusanyiko hiyo ya vijiwe wakiwa wameketi kwenye vigoda na mikeka huku kipaumbele zaidi kikiwekwa kwa makundi maalumu ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Prudence, alisema kaulimbiu ya Wiki ya AZAKi mwaka huu, ni "Sauti, Dira, Thamani" ikijikita katika kuwahimiza watu wote kuleta maendeleo katika nchi yao pamoja na kuwahimiza watendaji katika kuleta maendeleo.



Diwani wa kata ya Loiborsiret, wilayani Simanjiro, Ezekiel Maridadi (katikati) na Chifu wa mkoa wa Manyara, Alais Koina (kulia), wakimpongeza mdau wa maendeleo Taiko Ole Kulunju kwa kununua matangi mawili ya maji kwa ajili ya matumizi ya wananchi wa kijiji cha Oltepeleki, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Kanuni mpya ununuzi wa umma zaiva

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imepanga kuanza kutumia Kanuni za Rufani za Ununuzi wa Umma Julai Mosi, mwaka huu.

Aidha, mamlaka itatumia mfumo wa kuwasilisha malalamiko na rufani zitokanazo na michakato ya ununuzi wa umma lengo likiwa ni kuboresha eneo hilo.

Katibu Mtendaji wa PPAA, James Sando, alibainisha hayo jana jijini hapa wakati wa kikao kazi cha kupokea maoni ya uandaaji wa Kanuni za Rufani za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 katika utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi Umma ya Mwaka 2023.

Sando alisema Sheria Na.10 ya Ununuzi wa Umma ilitungwa na kupitishwa na bunge Septemba, 2023 na kwamba ili itumike vizuri, inategemea kanuni za ununuzi ambazo ziko katika hatua mbalimbali na zitakamilika na kuanza kutumika rasmi mwaka ujao wa fedha.

"Sheria iko tayari lakini haiwezi kutumika bila kuwa na kanuni ndiyo maana tupo hapa kwa ajili ya kupokea maoni ya wadau wa ununuzi kuhusu Kanuni za Rufani za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 ili kuiwezesha Sheria ya Ununuzi Umma ya Mwaka 2023," alisema Sando.

Aliongeza kuwa anaamini sheria hizo, zitapunguza changamoto kwenye rufani za ununuzi zilizokuwapo awali ambazo zilikuwa zinalalamikiwa na wazabuni.

Alisema baada ya kikao kazi kilichowakutanisha wadau wa ununuzi kutoka taasisi za umma, PPAA itaandaa kikao kingine na wazabuni ili nao watoe maoni yao kuhusu Kanuni za Rufani za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 kabla ya sheria hiyo kuanza kutumika rasmi.

Kamishna wa Sera ya Ununuzi wa Umma kutoka Wizara ya Fedha, Dk. Frederick Mwakibinga, ambaye alimwakilisha Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Jenifa Omolo, alisema serikali imefanya maboresho makubwa katika sheria hizo, hivyo watu watarajie mageuzi makubwa.

Dk. Mwakibinga alisema baada ya kanuni kukamilika, zitasaidia wananchi hususani wazabuni na wadau wa ununuzi kwenda kutumia kanuni ambazo zimekamilika na kuboreshwa na kuisaidia serikali kupata thamani halisi ya fedha katika miradi mbalimbali.

Alisema Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 10 ya mwaka 2023 imeboresha masuala mbalimbali ikiwamo kupunguzwa kwa muda wa kushughulikia malalamiko na rufani zinazotokana na michakato ya ununuzi wa umma.

"Mfano, muda wa siku saba za kazi kwa ajili ya kusubiri malalamiko ya wazabuni (cool off period) kabla ya kutoa tuzo umepunguzwa na kuwa siku tano za kazi. Muda huo hautajumuisha njia za ununuzi ambazo hazihitaji ushindani kama vile 'single source', 'minor value procurement' na 'shopping'.


"Kadhalika muda wa ofisa masuhuli kushughulikia malalamiko ya zabuni umepunguzwa kutoka siku saba za kazi hadi siku tano za kazi pale ambapo hataunda jopo," alisema Dk. Mwakibinga

Aidha, Dk. Mwakibinga alisema kutokana na maboresho hayo, endapo ofisa masuhuliataunda jopo la mapitio ya malalamiko, atakuwa na siku saba za kazi na atatakiwa kuwajulisha washiriki wote wa zabuni juu ya uundwaji wa jopo hilo. Sambamba na hilo, alisema muda wa PPAA kushughulikia malalamiko au rufani umepunguzwa kutoka siku 45 hadi 40.

"Ili kuwezesha utekelezaji wa Sheria Mpya ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023, PPAA iko katika mchakato wa kuandaa Kanuni za Rufani za Ununuzi wa Umma za mwaka 2024. Pamoja na mambo mengine, kanuni hizo zitatoa wigo mpana wa kuwasilisha malalamiko. Mabadiliko hayo yatawapa wazabuni fursa ya kushindana kwa haki na uwazi katika zabuni mbalimbali," alisema.

## KABWELA

**Na Fadhil Mohammed**



# Mil. 800/- kuwainua kiuchumi vijana

**Na Mwandishi Wetu**

DOLA za Marekani 300,000 (Sh. milioni 800) zitatumika kuwainua kiuchumi vijana kutoka mikoa mitatu nchini katika ushirikiano mpya kati ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) na Taasisi ya CRDB Bank Foundation.

Katika kuongeza ujumuishi wa wananchi kiuchumi hasa makundi maalum, taasisi hiyo imetia saini mkataba wa makubaliano kushirikiana na UNFPA kuwawezesha kiuchumi vijana wa umri wa kuanzia miaka 18 hadi 24 walioko shuleni na wale ambao wameacha shule kutokana na sababu mbalimbali.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa hafla ya kutia saini mkataba huo wenye thamani ya Dola 300,000 za Marekani (Sh. milioni 800) jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation, Tully Mwambapa alisema ushirikiano huo unatokana na kufanana kwa malengo na mipango ya pande zote mbili katika kuwezesha vijana kushiriki kikamilifu katika shughuli za uchumi.

"Tangu kuanzishwa kwake mwaka 2023, Taasisi yetu ya CRDB Bank Foundation tumeelekeza nguvu kubwa katika kuanzisha programu za kuwawezesha vijana na wanawake kujumuishwa kwenye mfumo rasmi wa huduma za fedha, kuwapa mafunzo na mitaji wezeshi kupitia Programu yetu ya Imbeju. Ushirikiano huu na UNFPA unakwenda kuimarisha jitihada hizi na kuwezesha kufikia vijana wengi zaidi," alisema Tully.

Kama ilivyo kwa taasisi hiyo, UNFPA inatekeleza programu tofauti za kuinua wananchi kiuchumi, kuwajengea uwezo wa kuzitambua haki zao, kupunguza migogoro ya kifamilia na kijinsia pamoja na kutoa elimu ya uzazi kwa wanawake, mabinti na vijana, azma ikiwa ni kujenga vijana wenye uwezo wa kiuchumi kukabili changamoto za kila siku.

Tully alisema ushirikiano huo unalenga vijana walio masomoni na wale walioshindwa kuendelea na masomo kutokana na sababu mbalimbali, watu wenye ulemavu pamoja na mabinti waliopata ujauzito wakiwa masomoni.

Katika utekelezaji wake, alisema wanakusudia kupunguza changamoto za upatikanaji ajira, kuwapa elimu ya fedha, kuwapa elimu ya afya ili kupunguza mimba za utotoni, kupunguza ukatili wa kijinsia na maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi (VVU) katika mikoa mitatu ya Dar es Salaam, Dodoma na Kigoma.

"Ushirikiano wetu na UNFPA utajikita kwenye maeneo mawili ya msingi. Kwanza ni kutoa elimu na maarifa ya kujitambua kwa vijana walio shuleni na walioa nje ya shule itakayojumuisha mafunzo juu ya huduma rafiki za afya, unyanyasaji kijinsia na jinsi ya kuepuka na namna ya kuishi na maambukizi ya VVU.

"Eneo la pili ni kutoa elimu ya fedha na ujasiriamali kwa vijana na mabinti ili kuwajengea mazingira ya kutekeleza majukumu yao kikamilifu," Tully alieleza.

Mark Bryan Schreiner, Mwakilishi Mkazi wa UNFPA nchini, alisema shirika hilo limekuwa linatekeleza miradi tofauti inayolenga kuwainua wananchi hasa wa makundi yaliyosahaulika katika jamii ili kuwa na uchumi jumuishi na wanufaika wakubwa wa programu zake ni wanawake, vijana wakiwamo mabinti wenye rika la balehe na wahamiaji wanaoomba hifadhi kutokana na migogoro ya kisiasa na kijamii inayotokea kwenye mataifa jirani.

"Tukiangalia changamoto zinazowakabili vijana nchini ikiwamo upatikanaji mitaji, ukosefu wa ajira na elimu ya ujasiriamali, UNFPA inayo kila sababu ya kushirikiana na wabia wa kimkakati kusaidia kuwezesha vijana nchini kushiriki kujenga uchumi wa taifa lao," alisema Schreiner.

Alisema UNFPA inatekeleza programu yake ya tisa nchini inayohamasisha uzazi salama kwa kuitambua na kuikubali kila mimba inayopatikana pamoja na kumwezesha kila kijana kutimiza ndoto za maisha yake.

"Lengo letu ni kuhakikisha hakuna anayeachwa nyuma, hivyo tunashirikiana na wadau wenye mtazamo kama wetu kama ilivyo Taasisi ya CRDB Bank Foundation," alisema Schreiner.

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, zaidi ya nusu ya Watanzania ni vijana wenye umri chini ya miaka 24.

Matokeo ya sensa hiyo pia yanaonesha asilimia 44 ya watu wote ni watoto wenye umri chini ya miaka 15 huku asilimia 19 wakiwa vijana wenye umri wa kuanzia miaka 15 hadi 24. Ndiyo idadi kubwa ya wananchi watakaoguswa na mradi huo wa kwanza wa ushirikiano kati ya CRDB Bank Foundation na UNFPA.

## Mlonganzila yatenga eneo la helikopta kutua

**Na Christina Mwakangale**

MKURUGENZI Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Prof. Mohamed Janabi amesema hospitali hiyo inaandaa eneo maalum kwa ajili ya helikopta kutua ili kuimarisha huduma za dharura.

Kutekeleza mpango huo, amekutana na kufanya mazungumzo na wataalamu kutoka Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) kwa lengo la kujadiliana na kuangalia eneo maalum litakalofaa kwa ajili ya helikopta kutua.

Amesema lengo ni kurahisisha kutoa matibabu kwa wagonjwa watakaokwenda kutibiwa hospitalini huko.

Kwa mujibu wa Prof. Janabi, MNH Mloganzila ni hospitali ya kisasa yenye miundombinu rafiki na kwa hadhi yake ya Hospitali ya Taifa, hivyo ni muhimu kuwa na eneo kama hilo ili ikitokea wagonjwa wanaohitaji huduma za dharura kunakuwapo mazingira rafiki zaidi ya kufika hospitalini kulinganisha na usafiri wa barabarani.

"Eneo ambalo lilikuwa linatumika Muhimbili kwa sasa si rafiki kutokana kuwa na majengo marefu, hivyo wataalamu hao wameona ni vyema wakafika MNH Mloganzila ili kuona mazingira na kisha kufanya uamuzi na hatimaye kutengeneza eneo maalum la kushukia helikopta," alisema Prof. Janabi jana jijini.

Pius Kazeze, Meneja Uendeshaji Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) jijini, alisema wameridhika na eneo ambalo wameliona kwa kuwa ni kubwa na linafaa ingawa kuna vitu vya kitaalamu ambavyo vitafanyiwa kazi.




Wauza juisi ya miwa, wakiandaa bidhaa hiyo, kwenye mazingira machafu ndani ya Stendi ya Mabasi ya Tegeta Nyuki, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam jana, kitendo kinachohatarisha usalama wa afya za wateja wao. **PICHA: JOHN BADI**

## TCRA yataka wabunifu watumie fursa zilizopo uchumi wa kidijiti

**Na Mwandishi wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano (TCRA) imewataka wabunifu katika sekta ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kuchangamkia fursa zinazotolewa katika utekelezaji miradi ya uchumi wa kidijiti.

Mkurugenzi wa TCRA, Dk. Jabir Bakari alitoa rai hiyo juzi alipozungumza na wabunifu, akieleza kuwa mamlaka hiyo inatoa bila malipo na kwa vipindi maalum rasilimali muhimu za mawasiliano kwa wabunifu na wajasiriamali wanaojitokeza kwenye TEHAMA na huduma za posta na usafirishaji vifurushi.

"Fursa tunazotoa ni namba, masafa na kikoa kinachoitambulisha Tanzania kwenye intaneti, yaani dot tz ambazo hutolewa kwa miezi mitatu (siku 90), ili kuwawezesha waombaji na kuchagiza ubunifu," alisema.

Dk. Bakari alisema mfano wa namba zilizotengwa na TCRA ni zinazotolewa bure ni msimbo wa *146*XX.

Dk. Bakari aliongeza kuwa TCRA inaendelea kuangalia mazingira yanayoweza kuchagiza mzunguko wa maisha ya wabunifu na wajasiriamali wanaojitokeza kwenye TEHAMA, ili ubunifu wao uwezeshe biashara huru zenye mafanikio.

Mkurugenzi Mkuu alisema maadhimisho ya Siku ya Wasichana na TEHAMA na Siku ya Kimataifa ya Mawasiliano na Jamii inayotumia TEHAMA yaliyofanyika nchini hivi karibuni yana umuhimu mkubwa wa kujenga jamii inayowezeshwa kidijiti katika upatikanaji huduma mbalimbali.



## Jela miaka 24 kwa kukutwa na meno ya tembo

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Babati, mkoani Manyara, imewahukumu watu wawili kwenda jela miaka 24 kila mmoja, baada ya kutiwa hatiani kwa kosa la kukutwa na meno ya tembo yenye thamani ya Sh. milioni 49.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Victor Kimario.

Waliohukumiwa kutumikia kifungo hicho, ni Fred Meibuko (28), mkazi wa Mvugwe, mkoani Tanga na Issa Mafita (30), mkazi wa Kijiji cha Gedamala kilichopo Kata ya Gallapo wilayani Babati.

Hakimu Kimario, alisema washtakiwa hao walikuwa wanakabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi, ambapo Novemba 4 mwaka jana, walikamatwa na jino moja la tembo, wakiwa wanatokea maeneo ya Singe Majengo Arusha na kukamatiwa Gallapo.

Alisema washtakiwa walitenda kosa hilo kinyume na Kifungu cha 86(1) na (2) (b) cha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283 ya Sheria iliyofanyiwa Marejeo Mwaka 2022, ikisomwa pamoja na Sheria ya Uhujumu Uchumi Aya ya 14, Kifungu cha 57 (1) na Kifungu cha 60 (2), Sura ya 200 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2022.

Aidha, alisema askari polisi walipata taarifa za washtakiwa hao kuwa wanasafirisha jino la tembo kutokea Gallapo, ndipo waliweka mtego na saa 6:00 mchana wakawakamata maeneo ya Gallapo.

Alisema baada ya kuwakamata alitwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Gallapo ili ashuhudie wakati wakiwapekua na baada ya kuwapekua walisaini hati ya mali na kupelekwa kituo cha polisi.

Vilevile, alisema shahidi namba moja aliwasilisha kielelezo ambacho ni jino la tembo na pikipiki iliyokuwa ikisafirisha jino hilo.

Kimario, alisema upande wa mashtaka walithibitisha pasina shaka kuwa washtakiwa walikamatwa na jino la tembo wakilisafirisha.

Alisema ameamua kuwatia hatiani kwa kuwa wao walikiri kuwa walikamatwa ila hawakuwa na jino la tembo bali walikuwa na kitu kingine ambacho walishindwa kukitaja, ndipo mahakama ikaona walitaka kujinusuru wasifungwe ila wao ndio walikuwa wanasafirisha jino hilo.

# Polisi wapewa pikipiki kuendeleza sekta ya utalii

**Na Beatrice Shayo,** ARUSHA

JESHI la Polisi mkoani Arusha limekabidhiwa pikipiki 20 zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 65 na Benki ya NMB zitakazosaidia kuimarisha ulinzi mkoani Arusha.

Mchango huo unaendana na mpango mkakati wa benki hiyo wa kuendeleza sekta ya utalii unaolenga kuimarisha mifumo endelevu ya ikolojia ya utalii.

Akizungumza wakati wa hafla ya makabidhiano ya pikipiki hizo iliyohudhuriwa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda katika Tawi la NMB Clock Tower, jijini Arusha juzi, Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi alisisitiza dhamira ya benki hiyo kuendelea kufanya kazi kwa karibu na wadau wote, ikiwamo serikali kusaidia maendeleo ya sekta ya utalii.

"Kwetu Mkoa wa Arusha ni muhimu na ni wa kimkakati kwa kuwa ni kitovu cha utalii kwa taifa letu. Na ndio maana leo (juzi0 tupo mahali hapa kukabidhi pikipiki 20 ili kuimarisha usalama. Kama benki, tunaamini kwamba usalama ukiimarishwa, sekta ya utalii itastawi kwa kiwango kikubwa," alisema.

Mponzi alionyesha matumaini kuwa juhudi za benki hiyo mkoani Arusha zitakuwa na athari kubwa zaidi katika mnyororo wa thamani wa sekta ya utalii nchini kote.

"Juhudi zetu zitakuwa chachu ya ukuaji wa sekta ya utalii kwa ujumla. Tunaamini kuwa watalii wakiwa salama hapa Arusha kama kitovu cha utalii, basi watakuwa tayari kwenda kufurahia utalii katika maeneo mengine nchini kama vile Zanzibar," Mponzi alisisitiza.

Mwenyekiti wa Chama cha Waongoza Watalii Wazawa nchini, Samuel Diah wakati wa hafla hiyo aliipongeza Benki ya NMB kwa mchango huo akionyesha imani kuwa kwa kiasi kikubwa utachochea ukuaji wa sekta ya utalii mkoani humo.

"Kwa kweli mchango huu umekuja wakati mwafaka kwani kuhakikisha usalama wa watalii wa ndani na nje ni kipaumbele kikuu kwetu kwa sasa.

"Juhudi za Benki ya NMB zitahakikisha usalama wa Mkoa wa Arusha wakati wote na vile utachangia juhudi za serikali kukuza sekta ya utalii. Usalama ndio kivutio kikubwa kwa watalii wote. Pamoja na Mkoa wa Arusha kuwa na vivutio vingi vya utalii, hatuwezi kuvutia watalii wengi kama mkoa hauko salama," alisema.

Diah alitumia hafla hiyo kumpongeza Mkuu wa Mkoa wa Arusha kwa kuanzisha kampeni ya kuliwezesha Jeshi la Polisi kupata pikipiki, huku akisisitiza kuwa mpango huo utaongeza ufanisi wa jeshi hilo katika utoaji huduma.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda wakati wa hafla hiyo, alisema serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan imekuwa mstari wa mbele katika kutangaza vivutio vya kipekee vya Tanzania na kuwataka wananchi kulinda vivutio hivyo vya utalii.

"Hili ni tukio la kihistoria na hakika ni ishara ya kurudisha kwa jamii. Wananchi wanatakiwa kusaidia kampuni zinazowajibika kama Benki ya NMB.

"Pikipiki ambazo zimetolewa leo hazitasaidia Jeshi la Polisi bali jamii nzima ya Mkoa wa Arusha kwani zitasaidia kuimarisha ulinzi na kuhakikisha usalama wa raia na mali zao," alisema.

Makonda alitoa wito kwa wakazi wote wa Mkoa wa Arusha kuendela kushirikiana kwa karibu na Jeshi la Polisi kuwabaini wahalifu wote mkoani mwao.




Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda (kulia), akifafanua jambo kwa viongozi waandamizi wa Benki ya NMB, baada ya kupokea msaada wa pikipiki 20 kutoka benki hiyo, kwa ajili ya kuimarisha ulinzi katika sekta ya utalii, jijini Arusha jana. Wa (pili kulia) ni Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki hiyo, Filbert Mponzi, Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kaskazini, Baraka Ladislaus (wa pili kushoto) na Meneja Mahusiano Huduma za Serikali wa NMB Kanda hiyo, Peter Massawe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi 23,000 wafungiwa mita za maji

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

SHIRIKA la WaterAid limewafungia mita za maji wananchi 23,000 katika Mkoa wa Manyara na Arusha.

Hayo yameelezwa jana jijini Arusha na Mkurugenzi Mkaazi wa Shirika la WaterAid Tanzania, Anna Mzinga.

Kwa mujibu wa Mzinga, mwaka 2018 waliingia ubia na kampuni ya EwaterPay na kufunga mita za malipo ya awali katika Kijiji cha Saranga kilichopo mkoani Manyara.

Alisema katika kijiji hicho wamewafungia wananchi 2,000 na mwaka 2021 katika mradi wa maji vijijini vitano Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha walifungiwa mita za maji za malipo ya kabla na kufikia jumla ya wananchi 23,000.

Mzinga alisema katika miradi hiyo miwili mwananchi ana uwezo wa kujaza fedha katika simu yake ili kulipia tokeni maalum inayotumika kuchotea maji kwa gharama ya Sh. 30 kwa ndoo yenye ujazo wa lita 20 fedha ambayo huingia kwenye kikundi cha watumiaji maji CBWSO.

"Miradi mingine iliyotekelezwa kwa ubunifu huo ni pamoja na mradi wa Bwawa la Maji Kwamaizi na Itigi mkoani Singida,"

Aidha, alisema wanaipongeza serikali kwa kuasili mfumo huo wao wanaamini katika ubunifu ni moja ya nyenzo muhimu wanayoitumia katika kutekeleza na kuwasilisha miradi yao.

"Tutaendelea kuunga mkono juhudi za serikali katika kubuni miradi mipya inayotumia teknolojia na kuifanyia tathmini zitakayorahisisha kujifunza na hatimaye kuleta matokeo chanya ya upatikanaji wa maji hasa katika kumtua mama ndoo kichwani,"

Mzinga alisema Shirika la WaterAid moja ya malengo waliyojiwekea imejipanga kujikita kimkakati katika Wilaya ya Hanang' mkoani Manyara katika kipindi cha utekelezaji wa mpango huo.

Alisema utekelezaji katika wilaya hiyo utasaidia kuonyesha mifano hai ya utekelezaji, ubunifu na ushirikishwaji ambao unaweza kusaidia kumfikia kila mwananchi na huduma endelevu na salama za maji, usafi wa mazingira na usafi binafsi jambo ambalo linaweza kuigwa katika maeneo mengine.

Waziri wa Maji, Juma Aweso, akiwasilisha Bajeti ya Wizara ya Maji Mwaka 2024/25 alisema matumizi ya mita za maji za malipo ya kabla zitaongeza ufanisi wa matumizi ya maji pamoja na kudhibiti kuvuja maji kunakosababisha hasara kwa mteja.

Alisema kupitia mamlaka za maji na Jumuiya za Watumiaji wa Maji (CBWSOs) zimeendelea kuwafungia wateja ambapo hadi Aprili 2024 wateja 13,526 walipatiwa huduma hiyo katika mikoa ya Dodoma, Iringa na Tanga.



# Madiwani watajwa kukwamisha ukusanyaji mapato Misungwi

**Na Remmy Moka,** SAUT

BAADHI ya madiwani na viongozi katika Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi wametajwa kuendekeza siasa na kuwa kikwazo katika ukusanyaji kodi, hali inayokwamisha juhudi za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Kufuatia hali hiyo, juzi katika kikao cha baraza hilo cha robo ya tatu ya mwaka 2023/24, Mkuu wa Wilaya hiyo, Johari Samizi alikemea vitendo hivyo na kuwataka madiwani hao kuwa wamoja na kushiriki kikamilifu katika ukusanyaji mapato.

Alisema hatua hiyo itasaidia halmashauri kufikia malengo ya ukusanyaji waliyojiwekea kwa mwaka, kwamba mpaka sasa tayari wamekusanya zaidi ya asilimia 80.

Aidha, aliwataka wataalumu wote wa sekta mbalimbali ndani ya wilaya kuhakikisha wanafanya usimamizi wa karibu katika kuhakikisha kodi inayokusanywa inatumika katika makusudio lengwa kwani baadhi ya watumishi wanafanya kazi chini ya kiwango.

Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Abdi Makange alisema ili madiwani wawe na taswira njema kwa wananchi ni lazima wasimamie fedha kwa uaminifu na kuhakikisha asilimia 40 ya makusanyo inatumika katika miradi ya maendeleo.

Pia alisema wanapaswa kutambua kuwa pasipo makusanyo bora na usimamizi imara wa kodi hawawezi kufikia lengo la uletaji maendeleo.

Diwani wa Viti Maalumu Kata ya Masasi, Dotto Nuwisha, alisema wananchi wengi wanahitaji kulazimishwa na namlaka husika ili kulipa kodi kutokana na uelewa mdogo juu ya suala hilo, kuitaka TRA kupeleka elimu kwa wananchi hao.

Diwani wa Kata ya Sumbugu, Jokoli Mayombo alisema TRA wanapaswa kuendelea kutoa elimu mara kwa mara na kutambua kuwa kutokuwashirikisha wafanyabiashara kuhusu umuhimu wa kodi ni moja ya kikwazo katika ukusanyaji mapato.



Daktari wa magonjwa ya meno katika Hospitali ya wilaya ya Muheza ya Samia Suluhu, mkoani Tanga, Musa Amini (kushoto), akitoa elimu ya kinywa na meno kwa wagonjwa waliofika hospitali hiyo, juzi. Huduma ya meno imeboreshwa hospitalini hapo, baada ya Serikali kuleta vifaa vya kisasa ikiwemo X-ray ya meno. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## 560 mbaroni tuhuma kuua, kubaka, dawa za kulevya

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

JESHI la Polisi mkoani Geita linawashikilia watu 567 kwa tuhuma mbalimbali ikiwemo mauaji, ubakaji na kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita SACP, Safia Jongo, aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari akisema watuhumiwa hao walikamatwa baada ya kufanyika kwa msako katika kipindi cha Aprili.

SACP Jongo alisema msako huo pia ulikamata mali za wizi ikiwemo mashine moja ya kusaga mawe, jenereta, cherehani mbili, televisheni, redio, pikipiki nane, magodoro nane pamoja na sola.

Aidha, alisema watuhumiwa hao wanatarajiwa kupandishwa kizimbani pindi ushahidi utakapo kamilika ili wakajibu tuhuma zinazowakabili.

Kuhusu usalama barabarani, Kamanda Jongo alisema, jeshi hilo limekamata watuhumiwa waliohusika katika makosa 8,124 ya ukiukwaji wa sheria na taratibu za barabarani.

Alisema watuhumiwa hao walipigwa faini, huku wengine wakifikishwa mahakamani.

Aidha, aliwataka wananchi mkoani hapa kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kuhakikisha wanafichua na kutoa taarifa za vitendo vya ukatili vinavyotekelezwa katika jamii.

SACP Jongo alisema matukio hayo yameendelea kukua kila siku mkoani hapo, huku wanaotekeleza matukio hayo wakitajwa kuwa watu wazima, lakini wamekuwa wakifichiwa siri hali inayosababisha matukio hayo kuendelea kuongezeka.

## Polisi watakiwa kuzingatia nidhamu, haki, uadilifu

**Na Vitus Audax,** MWANZA

KAMISHNA wa Operesheni na Mafunzo wa Jeshi la Polisi, CP Awadhi Juma Haji amewataka askari polisi kuzingatia maadili katika utekelezaji wa majukumu yao, ili kutoa haki kwa kila mwananchi.

Alitoa wito huo juzi jijini Mwanza wakati akizungumza na maofisa, wakaguzi wa jeshi hilo, kuwataka kuzingatia mambo muhimu manne katika shughuli zao ili kutekeleza majukumu yao kwa weledi wa juu zaidi.

Alitaja mambo hayo kuwa ni pamoja na nidhamu, haki, weledi na uadilifu na kuwa Jeshi hilo halipo tayari kuvumilia ukiukwaji wa maadili kwa namna yoyote utakaofanywa na askari.

"Suala la ukiukwaji maadili kwetu lina 'zero tolerance' (halivumiliki) hatuna mzaha wala huruma kwenye suala la nidhamu, hivyo zingatieni suala hilo" alisisitiza CP Awadhi.

Aliongeza: "Lakini niwapongeze kwa kazi nzuri mnayoendelea kuifanya katika kuimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao mkoani hapa kwani mnaufanya mkoa kuwa salama".

## Mama atelekeza watoto kisa ugumu wa maisha

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKAZI wa Iselamagazi wilayani Shinyanga, Hollo Dotto anadaiwa kutelekeza watoto wake wawili na kukimbilia mkoani Mpanda.

Watoto hao wenye umri wa miaka 13 na mwingine 12 wanatajwa kuishi maisha magumu ya kuomba mabaki ya chakula katika vibanda vya migahawa ya maeneo hayo.

Akizungumza na Nipashe kuhusu mkasa huo, Mwenyekiti wa Jukwaa la Wanawake Kata ya Iselamagazi, Zainab Jilumbe alisema hali hiyo imesababisha watoto hao kuacha shule na kuendelea na maisha ya mitaani.

"Baada ya kuwaona watoto hawa wakirandaranda mitaani na kula ukoko kwenye vibada vya kuuza vyakula tukaanza jitihada za kumtafuta tukishirikiana na serikali hadi tukampata akiwa Mpanda," alisema Zainab.

Alisema walipomuhoji alieleza kuwa amewatelekeza watoto wake kutokana na ugumu wa maisha, kwamba amekwenda Mpanda kutafuta vibarua vya mashamba kwa ajili ya kupata pesa.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Kata ya Iselamagazi, Joyce Chawala, alisema hali ya utelekezaji watoto kwenye kata hiyo imekuwa ikijirudia, kwamba mwaka jana pia kuna mtoto mmoja alitelekezwa nje ya nyumba ya mtu kisha mama yake kukimbia kusikojulikana hadi sasa.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Iselamagazi, Emmanuel Humba, alisema wamekuwa wakitoa elimu kwa wananchi kwenye mikutano ya hadhara juu ya kutelekeza watoto lakini jamii wamekuwa wagumu.

Alisema kwa sasa wanachokifanya ni mzazi akitelekeza watoto wanawatafuta ndugu zao na kuwapelekea kuishi nao.

Ukurasa 12



Ufugaji nyuki unavyochachamaa visiwani, ukiungana na Uchumi Buluu kubadili maisha yao




**Viti maalum karne hii sasa tuvipe jicho la tatu**

Ukurasa 13

BUFE
IJUMAA MEI 24, 2024
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

## RC MPYA NA MTAJI WA RAIS...

# Chongolo aanza na ziara kukagua bilioni 32/- alizowekeza Samia kuugeuza mkoa

**Na Ibrahim Yassin, Songwe**

KATIKA mgawanyo wa pesa kitaifa, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, Sh. bilioni 32 kuendeleza miradi ya mkoani Songwe, Mkuu wa Mkoa mpya, Daniel Chongolo, akijumuisha ziara yake ya kwanza, akiikagua.

Ni miradi mkoani hapo, inayaotekekezwa kwa miaka mitatu sasa, ikitumia fedha hizo, hiyo wiki iliyopita, ambako akazungumza na wakazi, ikiendana na kuwashauri na kuagiza, pale alipoona kasoro.

Ni ziara yenye ajenda kuu, kujenga umoja na mshikamano katika juhudi za maendeleo, kukemea maovu na ukatili wa kijinsia, mila potofu, ubakaji, ukatili wa kingono kwa watoto, mimba na ndoa za utotoni, ubadhilifu wa fedha za umma na lishe duni.

Siku ya kwanza alianza kukagua Shule ya Wasichana ya Ileje, akigawa jezi na mipira kwa wanafunzi. Hata hivyo, akanika kasoro ya rekodi mbaya ya kuwapo wenye ufaulu daraja sifuri 100, katika matokeo ya mitihani ya kidato cha nne.

Hapo, akawaelekeza walimu na maofisa elimu kuhakikisha wanainga katika mikakati ya shule ya ufaulu darasa sifuri, wanafunzi wote waangukie lengo la madaraja ya kwanza na pili.

#### KILIO KUCHELEWA MIRADI

Miradi mingine aliyotembelewa ni ya elimu, afya, maji, miundombinu ya barabara na madaraja, Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Stamico na kituo cha forodha kilichopo mpakani mwa Malawi na Tanzania.



Ziara ya Mkuu wa Mkoa, Daniel Chongolo, kukagua moja ya madaraja yanayojengwa mkoani kwake.**PICHA ZOTE: IBRAHIM YASSIN.**

Baada ya hapo Chongolo aliyekwishakuwa mkuu wa wilaya mbili tofauti, kisha Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM), mahali alikoanzia akiwa ofisa, akitokea kwenye uandishi vyombo vya habari, akawa na mkutano nja umma, akipokea kero zao.

Kero kubwa inayoonekana ni kuchelewa kwa ujenzi wa mradi wa maji wa Itumba -Isongole na jengo la utawala, huku akitoa maelekezo ya kuhakikishwa miradi hiyo inakamilika kwa wakati, ukiwamo wa barabara na daraja kwenye Mgodi wa Stamico, miradi mingine ikionekana iko vizuri.



Mkuu wa Mkoa Songwe, Daniel Chongolo, akizungumza katika ziara yake kujitambulisha.

Aidha, anawasifu wananchi wa Ileje kulima mazao mengi akikosoa kasoro yao ni kutojua kuipangilia mlo kamili, akisema hali ya udumavu kwa watoto chini ya miaka mtano sasa ipo juu, akiwasihi wale vyakula mchanganyiko, iwafae kiafya.

Pia, Chongolo akawageukia uso wanaume wa Songwe, dhidi ya kasi yai kuwapa mimba mabinti, hasa wa masomoni, akaliagiza jeshi la polisi, kuhakikisha linawakamata watakaobainika kusababisha ujauzito, hasa wanafunzi kwa ajili ya hatia za kisheria, huu akiwasihi wazazi kutowaozesha watoto chini ya umri huo.

"Rais Dk.Samia ameleta fedha nyingi zaidi ya bilioni 32 katika kipindi cha miaka mitatu ya urais wake. Fedha hizo zimejenga miradi mingi ikiwamo ya elimu, lengo watoto wasome ili wawe viongozi wa baadae na si kuwaharibia Maisha. Nitakayembaini 'nitakula sahani moja' naye,"anasema.

#### MAENDELEO YA AFYA

Mganga Mkuu wa Mkoa Songwe, Dk. Boniface Kasululu, anaifafanua Ripoti ya Utafiti wa Kidemografia Mwaka 2022, kwamba kiwango cha huduma kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kimepungua, kutoka asilimia 43 hadi 31.9.

Analalamika kwamba, kiwan-

Inaendelea Uk 12

UCHUMI

# Ufugaji nyuki unavyochachamaa visiwani kivyake, ukiungana na Uchumi Buluu kubadili maisha yao

**Na Mwandishi Wetu, UNGUJA**

WADUDU nyuki wanaojulikana zaidi kuzalisha asali. Hadi sasa, kuna aina zaidi ya 20,000 duniani. Maarufu zaidi ni; Nyuki wa Kazi, ambao ni wa kike, waumbaji watafutaji 'malighafi' ya asali na wa kiume, wako katika uzazi zaidi.

Nyuki hao hufanya kazi pamoja kujenga mizinga na kuvuna nta kutoka kwenye maua.

**AINA NA UFUGAJI**

Tanzania ina aina mbili kuu za nyuki, Nyuki wanaouma. Hao wanapatikana katika maeneo ya mwambao, penye ukame na milimani. Kiasili ni wakali na wana uwezo wa kuzalisha lita mpaka 30 za asali kwa mwaka.

Nyuki wasiouma huishi ndani ya matundu chini ya matawi makubwa ya miti, kwenye vichuguu vya mchwa na hata chini ya mapaa ya nyumba.

Uzalishaji wao wa asali ni mdogo (wastani lita tano kwa mwaka). Inaaminika nyuki wasiouma, pia asali yao ina uwezo mkubwa kutibu maradhi, kuliko ya wanaouma. Nao wako katika makundi: Nyuki wa Kazi (Apis mellifera) na Nyuki wa Kiume (Drones).

Pia, kuna Malkia (Queen Bee) ambayemajukumu yake ni kuzalisha mayai na kuongoza 'koloni'. Anazalisha kemikali inayoitwa 'feromoni' inayowasaidia nyuki wengine kudumisha utaratibu wa 'koloni'.

**UFUGAJI NYUKI ULIVYO**

Ufugaji nyuki ni shughuli ya kudhibiti na kuendeleza makoloni ya nyuki kwa ajili ya kuzalisha bidhaa mbalimbali kutoka kwao.

Ingawa wamezoea bidhaa asali, kuna bidhaa nyingine ambazo zimekua faida kubwa kiafya, pamoja na maendeleo kichumi: Nta, sumu ya nyuki, maziwa ya nyuki, vumbi, supu yake na gundi.

Visiwani Zanzibar, kwenye utajiri wa fukwe, pia maarufu kwa ubora na tofauti wa asili yake. Jiografia na hali ya hewa visiwani, imekuwa chachu ya upatikanaji aina tofauti za asali.

Kwa sasa Zanzibar inatoa asali za karafuu, mchanganyiko wa maua, matumbawe na mikoko.

Ufugaji nyuki Zanzibar, sasa unahusu uzalishaji wa asali, nta, propolis, na mazao ya mizinga. Mbinu tofauti zinatumika, ikiwamo mizinga ya nyuki inayotengenezwa kienyeji kama vile mizinga ya magogo na vikapu vilivyofumwa.



Tukio la kukabidhiana vifaa vya kisasa vya kuvuna asali, kisiwani Pemba.

**SMZ INAVYOAMUA KUWEKEZA**

Kasi ya ufugaji nyuki Zanzibar zinaenea katika nyanja za uchumi wa ndani, ikiwamo uzalishaji asali. Pia, imekuwa ni chanzo cha mapato kwa wafugaji.

Asali Zanzibar imekuwa maarufu ndani na nje ya nchi, kutokana na ubora na upekee wake, hivyo kuongeza mapato ya wafugaji na kuchangia katika uchumi wa nchi.

Bidhaa za nyuki na ufujgaji wake, pia zinatoa bidhaa nyingine kama vile nta, sumu ya nyuki, maziwa ya nyuki, vumbi, supu pamoja na gundi, zinazonunuliwa kwa bei kubwa na matumizi yake ni muhimu.

Faida nyingine ya nyuki visiwani, inatajwa ni kuzalisha mimea inayosaidia kuzalisha mimea na uzalishaji vimelea vyake (poleni), zinachangia katika uzalishaji mazao kama matunda na mboga.

Vilevile faida nyingine ni ajira na kujiajiri. Ufugaji wa nyuki unaweza kutumika kama ni njia moja ya kutoa ajira kwa watu wa vijijini na pia kuwapa fursa ya kujiajiri kwa kuanzisha biashara ndogo ya ufugaji wa nyuki.

Ufugaji nyuki Zanzibar, pia unaangukia kwenye utalii na maendeleo endelevu. Huko Sekta ya Utalii, ambayo ni mtaji wa serikali yake kiuchumi, inafaidika na ufugaji nyuki kupitia Utalii wa Mazingira.

Ni eneo linalotajwa kuvutia wageni, wanaoupenda utalii wa kilimo na uhifadhi wa mazingira.

**NYUKI SASA BIASHARA**

Katika kuona umuhimu na faida zinazopatikana kwa kupitia ufugaji wa nyuki, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), imeanzisha taasisi inayisaidia kuwaandalia mazingira rafiki wajasiriamali ambao wangependelea kuwekeza katika sekta ya ufugaji wa nyuki.

Huyo ni Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar (ZEEA) ni taasisi iliyoanzishwa kisheria mwaka 2022.

Kurejea jina lake, taasisi linatajwa kuwa jukumu la kuwawezesha wananchi wajikwamue katika umaskini, kwa kutumia njia kuu nne.

Hapo zinaorodheshwa kuwa ni upatikanaji kirahisi mahitaji katika maeno yafuatayo: Mitaji; mafunzo ya bidhaa wa bidhaa na mbinu tofauti za ujasiriamali wanazozitengeneza; masoko ya bidhaa na huduma zinazotengenezwa na wananchi Zanzibar; na kutengenezwa sera rafiki kwa ajili ya wajasiriamali.

Taasisi hiyo katika tajwa, ina vituo vinne vya kutoa mafunzo, ambako ni wanaolea na kukuza wajasiriamali kilichoko Mbweni; Chuo cha Barefoot Kibokwa vyote vya Unguja; na Kituo cha Kutengenezea Asali Kizimbani; Kituo cha Kuchakata Asali cha Pujini, Pemba.

Fatma Juma, ni Mkurugenzi wa Uratibu wa Mafunzo na Miradi, anaeleza kwamba ZEEA imekusudia kuwekeza katika ufugaji nyuki, baada ya kuona mafanikio na faida inayorwejesha.

"Uwekezaji huu tumekuwa tukiufanya kuanzia hatua ya awali, inayohusu kutembelea maeneo mbalimbali ili 'kuwashajihisha' wananchi, kuhusu ufugaji wa nyuki.

"Kwa wale ambao watahamasika na sekta hii, tunawaorodhesha kwa ajili ya kuwapatia mafunzo kuhusu njia za kisasa za ufugaji nyuki," anasema.

Fatma anafafanua, kwa sasa taasisi yao imefanikiwa kutoa mafunzo kwa vikundi 59 Unguja na 86, Pemba, sambamba na kuwapatia vifaa vya ufugaji wanavikundi hao.

Anasema mpaka sasa, wanaofaidika na vifaa hivyo wako 663 wa Unguja na 941 wako Pemba.

"Tulifanya hivi baada ya kuona kuwa wafugaji wengi wa nyuki wanakosa mbinu za kisasa za ufugaji nyuki, programu za mafunzo, na vifaa bora." Fatma anaeleza.

Mratibu wa Wakala, ambaye ni Msimamizi wa Shughuli za ZEEA - Pemba Haji Haji, amekuwa mstari wa mbele kuwafuatilia na kuwatembelea wajasiriamali, kuwakagua mafanikio na changamoto zao katika uzalishaji na kuwatatulia inapobidi.

"Tumekuwa tukiwatembelea kila baada ya miezi miwili ambapo ili kuwatatulia changamoto wanazokutana nazo.

"Baadhi ya changamoto hizo ni uwepo wa wadudu na magonjwa, kama vile wadudu kama 'Varroa' na 'American foulbrood', ambao huleta tishio kubwa kwa makundi ya nyuki na uzalishaji wa asali.

"Lengo ni kuhakikisha kwamba wafugaji hawa wanazalisha asali na bidhaa nyingine za nyuki zikiwa katika ubora wa kimataifa," anasema Haji.

Brenda Ndosi, Msimamizi wa Kituo cha Mafunzo Kibokwa kilichopo Wilaya ya Kaskazini 'A' Unguja, anataja kituo chao kimekuwa kikifanya kazi mbili kubwa katika kuleta mapinduzi kupitia sekta hiyo ya ufugaji na uchakataji asali.

Utatuzi wake, anaeleza wanashirikiana na chuo, Barefoot College cha India, kituo hicho kikitoa mafunzo kwa kinamama, yakiwamo utengenezaji vifaa vinavyotumia umeme wa jua, kushona na elimu ya ufugaji nyuki.

Pia, imekuwa ikinunua asali inayotengenezwa kutoka kwa wafugaji hawa na kuitafutia masoko katika hoteli tofauti Zanzibar.

"Tumekuwa tukitoa mafunzo kwa ajili yao na pia tukinunua kila bidhaa waliyotengeneza na kuifanyia marekebisho kwa ajili ya kuipandisha thamani," anasema Brenda.

"Kwa sasa tunanunua asali za aina tofauti na kuziweka katika package ili kuziongeza thamani. Hii sio tu inawasaidia wazalishaji na wafugaji wa nyuki.

"Pia, inasaidia kutangazia utalii wa Zanzibar kwa kutumia asali yetu hii ambayo huwezi kuipata sehemu nyingine yoyote zaidi ya hapa.

'Ndio maana hata bei yake ni kubwa ukilinganisha na asali zinazotoka katika mikoa mengine nchi Tanzania." anaongeza Brenda.

Mkurugenzi Mtendaji Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Juma Mohammed, muumini wa mfumo wa: 'Niwezeshe nijitegemee' ulioko visiwani, anahitimisha akiwataka wananchi wake 'kuchungulia fursa' zinazotokana na ufugaji nyuki.

"Tumekuwa tukiona nchi nyingine jinsi wananchi wake wakitajirika kwa kupitia sekta hii. ZEEA iko tayari kumpatia mtaji yeyote ambaye atakuwa na mpango utakaowezesha uzalishaji wa bidhaa za nyuki na tutaendelea kuwatafutia masoko ndani na nje ya Tanzania," anasema Mohammed.



Kazi ya kuhudumia asali ikiendelea, Unguja. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

## CHONGOLO AANZA NA ZIARA KUKAGUA BILIONI 32/- ALIZOWEKEZA SAMIA, KUUGEUZA MKOA

Inatoka Uk 11

go hicho bado ni kikubwa, ikilinganishwa na kiwango cha kitaifa asilimia 30 na kiwango cha unyonyeshaji maziwa ya mama mkoa una asilimia 60.7, wakati kitaifa ni asilimia 59 na kupitia takwimu hizo, wanaendelea kutoa elimu ya kuhakikisha viwango ama vinashuka au kumalizika kabisa.

Anasema, katika kudhibiti latizo la lishe duni mkoani Songwe, wanatekeleza afua mbalimbali za kukabiliana na tatizo la lishe, ikiwamo kusimamia utekelezaji wa mkataba wa viashiria vya lishe na mpango mkakati jumuishi, kupinguza udumavu kwa 2021/2022 hadi 2025/2026.

Kutokana na hali hiyo mkuu huyo wa mkoa, anawataka wananchi kuunga mkono jitihada za serikali kuhakikisha mambo yote yana yokatazwa yanamalizika na kuufanya mkoa kuwa wa kihistoria kwa mambo mazuri na si mabaya.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Viti maalum karne hii sasa tuvipe jicho la tatu






NA JOSEPH KULANGWA
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com

SIKU chache baada ya kuingia madarakani Machi 19, 2021, Rais wa Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan alitamka kuwa yeye ni rais katika umbile la mwanamke.

Wapo waliojiuliza kwanini mama kasema vile, lakini alimaanisha kuwa urais haujali jinsia bali uwezo na dhamira ya kweli ya kuongoza watu wenye imani kwako.

Rais Samia 'Chifu Hangaya', alifanya hivyo baada ya kuwapo 'vijineno neno', hasa kwa kuzingatia kuwa ilikuwa mara ya kwanza katika historia ya nchi.

Lakini, aliwahakikishia kuwa anaweza na hakika ameweza kufanya, tena kayafanya kwa muda mfupi sana! Nchi imetulia na ujenzi wa taifa unaendelea kama ulivyoasisiwa.

Hivi sasa tunasikia kauli za 'Mama anaupiga mwingi!' Nani kama Mama!

Songa na Samia! Simama na Samia! Haya ni ya dhati na tofauti na yale ya wanaojiita wako naye kwa misamiati na majina tofauti. Kwa kifupi, hapana ombwe katika uongozi wa taifa la Tanzania,

yawezekana ni mpango wa Mungu, kwamba siku moja taifa litaongozwa na mwanamke na atafanya vizuri pengine kuliko hata wanaume. Nani anabisha?

Zamani, wapo hawakuamini mwanamke katika jinsia hiyo inaweza kufanya mambo hayo na ndiyo sababu utamaduni na mila zilimtenga katika kufanya uamuzi, pia katika kushiriki mikutano iliyojumuisha wanaume.

Kwa miaka hiyo, mwanamke mbali na kuzaa, alipewa jukumu la kulea familia, kupika, kunyonyesha na kukusanya kuni kama si kulima, huku mwanaume akicheza bao, karata, dhumna na michezo mingine akisubiri kula.

Hivi karibuni, katika maadhimisho ya Miaka 60 ya Muungano, tulishuhudia kwata ya Polisi Tarabushi ambalo tuliambiwa huko nyuma mwanamke hakuruhusiwa kujiunga na jeshi hilo, kisa jinsia!

Zamani mwanamke katika baadhi ya mila hakuruhusiwa kula maini, kula firigisi na vyakula vyovyote vile, vilivyoonekana kuwa vitamu na vizuri kwa afya. Vyote alipewa mwanaume kuwa ndiye alistahili mazuri yote.

Leo mwanamke anajiunga na jeshi lolote la ulinzi na usalama. Mwanamke ni msimamizi wa miradi ni mhandisi, anarusha ndege, anaendesha treni, basi, lori, meli, bajaji, bodaboda, pia akiendesha mashine au mitambo ya ujenzi.

Tumemuona mwanamke hivi leo anacheza mpira wa miguu kama ambavyo anacheza mwanaume. Baba naye anacheza netiboli kama anavyocheza mwanamke. Tunaona mwanaume anaoa mwanaume; ushoga!

Lakini, tunashuhudia mwanamke anaoa mwanamke; 'Tom boy', hali kadhalika mwanamke leo analea mumewe anayekaa nyumbani, huku mwanamke akitafuta riziki kwa kujiajiri, kuajiriwa na ujasiriamali.

Nani haoni kuwa mwanaume leo anasuka nywele na kuvaa herein, huku akitoga pua na kuweka kipini kama mwanamke? Tunaona wanaume wakivaa suruali za kubana kama waliyokuwa wakivaa wanawake zamani!

Mwanaume ni baba lishe kama alivyo mama lishe.

Yote haya yanaonyesha jinsi gani, sasa tofauti baina ya mwanamke na mwanaume inavyozidi kupungua na hatimaye itatoweka, ikiondoa dhana potofu kuwa mwanamke ni mnyonge mbele ya mwanaume na hivyo hastahili lolote.

Tukishabaini yote hayo na kukubaliana nayo, hatuna budi sasa kujiuliza kama kuna sababu ya kuendelea na kilio cha uwakilishi wa '50 kwa 50'baina ya wanawake na wanaume katika uwakilishi kwenye taasisi na vyombo mbalimbali.

Hivi kuna haja tena ya kuendelea kuwa na wabunge au madiwani wa viti maalumu, katika muktadha huu ambao hauonyeshi tena unyonge wa wanawake katika jamii? Bila shaka hapana sababu!

Kwa sababu, hivi sasa mwanamke anaweza kwenda jimboni au katika kata akagombea udiwani na ubunge bila wasiwasi, badala ya kusubiri mbeleko ya viti maalumu ambayo hutubebea hata wasio na uwezo ila sura na vifua.

Ni imani ya wengi kuwa, hivi sasa hata kama si mwaka huu au mwakani, siku zijazo tuondokane na dhana ya kutenga wanawake na kuwapa nafasi maalumu za uoingozi kwa kuzingatia jinsia na badala yake tupambane, kwa sababu tunaelekea kuwa sawa kwa asilimia 100.

Lakini, kufanya hivi, kutapunguza pia mzigo kwa Serikali kulipa mishahara na posho na marupurupu mengine kwa wabunge wa viti maalumu, na hivyo fedha hizo kufanya kazi zingine kwa malahi ya wananchi. Wanawake wanaweza au siyo?

## BIASHARA

# PPP - Elimu ya Mtandao, ilivyomrahisisishia rasilimaliwatu mwalimu kufunza darasani

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA madai ya kisasa ya maendeleom hugusa pia suala la vifaa bora kikazi, ikiwamo zinazogusa mageuzi ya kiteknolojia.

Inapoangukia katika jukwaa la utumishi, hilo limekuwa kilio kikubwa kwa jamii inayokusanyika. Inatajwa, katika sekta ya elimu na hasa watendaji wake wakuu walimu, nadharia inataja maendeleo ya teknolojia yanapotumiwa ipasavyo, suluhisho la kidijitali katika ufundishaji.


Pia, ndani ya maendeleo ya mfumo huru na shirikishi, baina ya umma na binafsi, maarufu 'PPP' (Public and Private Partnership) inatakiwa kutumika kikamilifu kufanikisha maendeleo hayo na tayario ina sheria na sera yake rasmi, maarufu kwa jina hilo la kifupi.

Nchini, kwa muda mrefu shule za umma zimekuwa zikikumbwa na changamoto za uhaba wa vitabu kukiwa na madarasa yenye wanafunzi wengi; wastani wa uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi ni 50:63 kwa shule za msingi, hata kuchangia mazingira ya kujifunza kwa wanafunzi na walimu kuwa magumu.

Sasa 'PPP' imezalisha mbadala. Tovuti za kidijitali zimewezesha kuweka masomo mbalimbali kwa njia ya mtandaoni na kurahisisha wanafunzi kujisomea kwa urahisi, baadala ya kutumika nguvu ya walimu muda na mahali popote.

Mwaka 2017 taasisi ya Vodacom Tanzania Foundation, ikiwa ni mbia wa PPP, ilianzisha mfumo 'E-Fahamu' kwa lengo la kusaidia wanaojifunza, upatikanaji wa masomo kwa njia ya kidigitali.

Tovuti hiyo inapatikana bila ya matumizi ya data kwa mtandao wa Vodacom, ambayo watu wanaweza kuitumia kupitia simu zao za mkononi au kompyuta.



Mwanafunzi akiendelea kusoma kupitia nyenzo ya e-Fahamu. **PICHA: MTANDAO**

Taasisi hiyo imetekeleza programu hii ya elimu mtandaoni katika shule tofauti nchini, ili kuboresha matokeo ya kujisomea kupitia nyenzo za kidijitali, kuleta mapinduzi ya namna walimu ya kufundisha na wanafunzi kujisomea na kuhakikisha inapatikana kwa wanufaika kupitia rasilimali tofauti kurahisisha kujifunza.

**WALIMU WACHEKELEA**

Akizungumza baada ya kuunganishwa na e-Fahamu katika Shule ya Sekondari ya Buhongwa ya mkoani Mwanza, Mwalimu wa TEHAMA, Paulo Getaro, anasema kuwa mfumo huu umekuja kurahisisha upatikanaji wa masomo ya kujisomea kwa wanafunzi.

"Hapo nyuma tulikuwa na njia moja tu ya upatikanaji wa masomo ambayo ni vitabu pekee. Kuja kwa e-Fahamu kumeturahisishia upatikanaji wake kwa wanafunzi wetu kwasababu masomo yote yanapatikana sehemu moja na yanaonekana kwa urahisi.

"Kwa mfano, wanafunzi huwa wanakuja kuulizia mazoezi yaliyomo kwenye mitihani iliyopita ili wajifunze. Inatuchukua muda kutafuta na pengine tusiipate lakini sasa hivi tunawaelekeza waingie kwenye tovuti hii," anaeleza Mwalimu Getaro.

Kuanzishwa programu hiyo katika shule ya Buhongwa, kumeongeza ari ya wanafunzi kujifunza kwa kutumia nyenzo za kidijitali.

Wamekuwa na shauku kufahamu namna vifaa kama vile kompyuta na intaneti zinavyorahisisha kujisomea. Ni hali inayotajwa sasa kuvutia wengi kuhudhuria masomo, kila wanapofahamishwa siku fulani watajifunza kwa kutumia vifaa hivi vya kisasa.

Mwalimu huyo anasema, matarajio waliyonayo kwa shule na wanafunzi baada ya kuwekewa mifumo na kupatiwa mafunzo ya e-Fahamu shuleni kwao, akinena "tuna mpango wa kuanzisha darasa la kompyuta ambalo litajumuisha wanafunzi wa kidato cha kwanza na cha pili.

"Tunaamini wanafunzi hawa kwa kuwa mbioni kusajiliwa kufanya mitihani ya kitaifa watakuwa chachu na mabalozi wazuri kwa wenzao kuitumia programu hii ipasavyo.

"Kwa sisi walimu pia tutaitumia vema tovuti hii na nyenzo tulizopatiwa na taasisi ya Vodacom ili kurahisisha ufundishaji wetu. Kwa sababu sasa itakuwa rahisi kutafuta masomo ya kufundisha na kuwaelekeza wanafunzi namna ya kuyapata. Lakini pia itarahisisha hata miongoni mwa wanafunzi kuwaelekeza wenzao." anasema

Tovuti ya e-Fahamu inatajwa kusaidia upatikanaji maktaba ya Mtandao ya Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE), video za katuni za TIE, Video za uchambuzi wa walimu zinazohusu masomo yanayolingana na mitaala.

Hapo inatajwa mifano ya chaneli kadhaa kwa wanafunzi wa shule za msingi kama; Chaneli Shirikishi ya Hisabati na SWayansi kwa shule za sekondari.

Taasisi hiyo inashirikiana na wadau kutoka sekta za umma na binafsi kueneza tovuti ya e-Fahamu kwenye shule za sekondari.

Mpaka sasa, taasisi hiyo inatajwa kupitia ushirikiano huo imewafikia wanafunzi zaidi ya 215,000 shule za sekondari na walimu zaidi ya 15,000 wamepatiwa mafunzo.

Kwa kuongezea, malengo ni kuziunganisha shule takribani 21 na e-Fahamu nchini kote ambazo zitawezeshwa kikamilifu na mifumo ya maabara za TEHAMA ikiwamo kuunganishwa na intaneti kutoka kampuni ya simu.

# BIASHARA – MAZINGIRA, MWEKEZAJI YAMWITIKIA DK. SAMIA AKIINGIZA SOKONI PIKIPIKI ZA GESI

**Na Frank Monyo**

NI SIKU chache tu, Dk. Samia Suluhu Hassan, alitoa maelekezo saba kuhusu nishati safi ikiwamo Wizara ya Nishati, kuhakikisha inaweka mazingira mazuri kwa wadau wa sekta binafsi kufika vijijini na kuweka vituo vya kujaza gesi.

Maelekezo hayo aliyatoa wakati wa hafla ya uzinduzi wa mkakati wa taifa wa matumizi ya nishati safi ya kupikia ya 2024 -2034 uliofanyika Dar es Salaam.

Rais Dk. Samia, moja ya maelekezo yake aliagiza Wizara ya Nishati ikae na wadau husika serikalini ikiwamo sekta ya fedha na mipango na binafsi kubaini maeneo ambayo yakifanyiwa kazi yataongeza upatikanaji wa nishati safi ya kupikia kwa gharama himilivu.

Hapo ni ualisia wa juhudi kubwa kukomesha kabisa matumzi ya nishati isiyo rafiki ya kupikia na ambayo inachochea kuharibu mazingira. Pia, Rais Dk. Samia akabainisha kuwa ifanyike tathmini ya athari za kimazingira, kiuchumi na kiafya.

Kutokana na hilo, Kampuni ya Watu Credit (Tanzania) imekuja na mkakati wa kuziba mianya ya uchafuzi wa mazingira kwa kutoa mikopo wezeshi ya vyombo vya usafiri ambavyo vinatumia gesi lengo likiwa ni kutunza mazingira.

"Dhamira ya Kampuni yetu ya Watu ni kumfikia kila Mtanzania popote alipo na tuna mpango wa kupanua wigo wa ukopeshaji wa pikipiki zinazotumia gesi asilia (CNG), bajaji na magari yanayotumia umeme" anasema Rumisho Shikonyi, Meneja Mkuu, Kampuni ya Watu Tanzania

Anaongeza kuwa; "Programu hii inalenga kuweka barabarani zaidi ya pikipiki 1,000 za matairi matatu ambazo ni rafiki kwa mazingira ifikapo mwishoni mwa mwaka 2024, na hivyo hatua hii ni ya kuhakikisha mazingira yanatunzwa kwa watu kuvuta hewa safi,"

Shikonyi, anasema kuwa hatua ya kampuni hiyo kutoa mikopo ya vyombo vya moto vinavyotumia gesi ya CNG ni kuongeza matumizi ya nishati safi na salama nchini.

"Sisi tunakuwa kichocheo cha ubunifu na ukuaji wa kiuchumi katika sekta ya usafiri wa kijani. Ukopeshaji wetu unawaendeleza wajasiriamali wanaotamani kuanzisha biashara, kuunda ajira mpya na kukua kiuchumi ndani ya Dar es Salaam na Tanzania kiujumla," anasema Anasema kuwa usambazaji wa magari ya umeme utachochea ajira na kutoa fursa za maendeleo kwa watengenezaji wa magari hayo, miundombinu na mafundi hivyo kuongeza mnyororo wa uchumi wa mto mmoja mmoja.

"Watu, tunaamini maendeleo endelevu ni zaidi ya kauli. Tunasaidia Dar es Salaam kujenga mustakabali wa kijani kwa kuja na mipango hii ya ukopeshaji wa kibunifu kwenye nishati safi.

Kupitia ushirikiano na watengenezaji, taasisi za serikali, na mashirika ya kijamii, tunajenga msingi mzuri wa kesho ya kijani kwa jiji letu," anasema Shikonyi





# WB: Hedhi bado mzigo kwa wanafunzi wa kike

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa amesema zoezi la urasimishaji linaloendelea maeneo mbalimbali nchini litaboreshwa ili kuleta ufanisi.

Silaa aliyasema hayo juzi wakati wa semina kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii juu ya utekelezaji Mradi Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi nchini (LTIP) hadi kufikia Mei 15, 2024 iliyofanyika Ukumbi wa Samwel Sitta, bungeni, jijini Dodoma.

Alisema maboresho hayo ya urasimishaji yatawafanya wananchi kuelewa kuwa kuishi eneo rasmi kama vile la mita za mraba 750, kuna faida zaidi kulinganisha na kuishi eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 1,000 lisilo rasmi.

Aliwataka wananchi wanaorasimishiwa maeneo yao kutekeleza dhana ya kujitolea wakati wa zoezi hilo kwa kuwa ndiyo dhana ya ujamaa na falsafa ya Tanzania inayomfanya mwananchi kuelewa sehemu ya eneo lake imetolewa kwa ajili ya matumizi ya huduma kama vile barabara, makaburi na shule.

Alisema utekelezaji huo ukifanyika, uvamizi kwenye maeneo ya wazi unaofanyika hivi sasa kwenye maeneo mbalimbali utapungua.

"Tunapopanga na kupima maeneo, mtu anapopata kiwanja chake basi ajue nina kiwanja eneo fulani lakini kuna maeneo ya umma ambayo yapo na wakati mimi ninapata kiwanja nimeyalipia," alisema Silaa.

Kwa mujibu wa Waziri Silaa kuna maelekezo kwa maeneo yanapopangwa na kupimwa kwamba mtu anaponunua kiwanja chake cha makazi ajue hawezi kuishi peke yake na atakuwa amelipia pia maeneo ya huduma kama vile ya kuabudu na kuzika.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda aliwaeleza wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuwa wizara imeendelea kutoa elimu hususan kwenye maeneo yanayomilikishwa kwa hati.

Alitolea mfano uwekaji mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji kuwa zoezi hilo limekuwa likihusisha wananchi wa maeneo husika huku akiweka wazi kuwa elimu imekuwa inatolewa kwa makundi mbalimbali ili kujua umuhimu na namna ya kutunza hati.

"Ushirikishwaji katika zoezi la mipango ya matumizi ya ardhi kwenye vijiji ni mkubwa sana maana wanaokwenda kusimama na zoezi ni wananchi wenyewe. Kwahiyo, utoaji elimu ni mkubwa na wananchi wanaelimishwa kwa makundi ili kuelewa hati inayokwenda kutolewa," alisema.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeendesha semina ya siku moja kwa wajumbe wa kamati hiyo kwa lengo la kuelezea hatua zilizofikiwa kwenye Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi Tanzania (LTIP) hadi kufikia Mei 15, 2024.

Mradi huo unatekelezwa kupitia vipengele vinne ambavyo ni kuongeza usalama wa milki za ardhi, kuimarisha mifumo ya taarifa za ardhi (ILMIS), kujenga miundombinu ya ardhi pamoja na kusimamia mradi.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Lucas Malia ya Ruangwa, kwenye viwanja vya Bunge jijini Dodoma, jana, aliowaalika kwenda bungeni kwa ziara ya mafunzo. **PICHA: OWM**

## CHADEMA: Tutawaengua walioshawishiwa kugombea

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimesema endapo kuna mwanachama ambaye ameshawishiwa kugombea uongozi kwa malengo fulani katika uchaguzi unaoendelea ndani chama hicho ataenguliwa.

Mwenyekiti wa Baraza la Vijana Chadema (BAVICHA), Patrick Ole Sosopi, alisema hayo juzi wakati akifungua mkutano mkuu maalum wa uchaguzi wa viongozi wa Jimbo la Singida Mjini.

"Aliyeshawishiwa kugombea kwa malengo ambayo yeye anayafahamu na yule aliyemshawishi tambua umepewa majukumu ya kutumikia chama hiki nenda kakitumikie na ukizingua tutakutoa," alisema.

Sosopi ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chadema, alisema watakaochaguliwa jukumu lao kubwa ni kuunganisha wanachama na chama kwenye mitaa, vitongoji na vijiji kwa ajili ya kujiandaa na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 ili chama kiweze kuibuka na ushindi.

Mwenyekiti wa Chadema Mkoa wa Singida, Emmanuel Jingu alisema uchaguzi wa viongozi unaofanyika katika majimbo yote ya mkoa huu utakwenda salama na kwamba hakuna viashiria vyovyote vya watu kupewa rushwa

Alisema jimbo la Singida Mjini limefanya vizuri katika usajili wa wanachama kidijitali ambapo wamesajiliwa zaidi 2,000 na kwamba jimbo hilo linatakiwa kuwa la mfano na kiongozi wa majimbo yote.

Alisema: "Chadema katika malengo ya kutaka kushika dola inalitegemea sana Jimbo la Singida Mjini kuyaongoza majimbo mengine, hivyo mnatakiwa kuchagua viongozi makini ambao watawasikiliza wananchi na uwezo wa kupaza sauti kudai haki".

**Aliyeshawishiwa kugombea kwa malengo ambayo yeye anayafahamu na yule aliyemshawishi tambua umepewa majukumu ya kutumikia chama hiki nenda kakitumikie na ukizingua tutakutoa.**

# EWURA yatoa elimu ya leseni ufungaji umeme

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) Kanda ya Kati, imetoa elimu kwa wanafunzi wa vyuo vya ufundi stadi vya Kongwa, Kihonda na Mikumi kuhusu utaratibu wa kuomba leseni za ufungaji mifumo ya umeme ili huduma bora na salama.

Akizungumza na wanafunzi hao wa fani ya umeme, Mhandisi wa Umeme Mwandamizi kutoka EWURA Kanda ya Kati, Nicholaus Kayombo alieleza kuwa leseni za ufungaji mifumo ya umeme hutolewa kwa mujibu wa Kifungu cha 8 cha Sheria ya Umeme, Sura ya 131 inayomtaka yeyote anayefanya shughuli za ufungaji mifumo ya umeme nchini kuwa na leseni ya EWURA.

"Ni muhimu wote kutambua kwamba suala la kuwa na leseni ni takwa la kisheria, hivyo ni lazima kuwa na leseni ili kutambulika na kufanya kazi stahiki inayoendana na ngazi ya elimu husika" alieleza.

Alibainisha kuwa EWURA imekuwa ikitoa elimu kwa makundi mbalimbali ya wadau wake ili kuimarisha uelewa wa masuala mtambuka kuhusu udhibiti wa huduma za nishati na maji ikiwamo kupokea malalamiko na kutatua migogoro inayotokana na huduma zinazodhibitiwa.

Alisema: "Maombi ya leseni za ufungaji umeme hufanyika mtandaoni kwenye mfumo wa LOIS, uliopo katika tovuti ya EWURA na mwombaji anapaswa kuwa na cheti cha mafunzo, picha ya pasipoti, kitambulisho (cha kura, NIDA au leseni ya udereva) na wasifu (CV)".



# Mama Samia Legal Aid yatatua migogoro 516

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Balozi Dk. Pindi Chana amesema migogoro 516 imetatuliwa kati ya 4,942 kupitia kampeni maalumu ya msaada wa kisheria ya Mama Samia Legal Aid bila ya gharama yoyote katika mikoa sita.

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uzinduzi wa kampeni ambayo itafanyika katika viwanja vya stendi ya zamani, mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Naibu Waziri Mkuu, Dk. Dotto Biteko.

Balozi Chana alisema hadi sasa mikoa sita imefikiwa na wananchi 415,000 wamehudumiwa.

"Kampeni hii inatarajiwa kutekelezwa katika halmashauri zote za Mkoa wa Njombe na tayari Mkuu wa Mkoa ameshajipanga na timu yake ikijumuisha kata 60 na vijiji 180 kwa kipindi cha siku 10 kuanzia Mei 26 hadi Juni 04 Juni," alisema Balozi Chana.

Alisema kampeni hiyo itahusisha utoaji elimu kuhusu masuala mbalimbali ya kisheria ikiwemo ardhi, haki za binadamu na utawala bora, mirathi, ndoa, ukatili wa kijinsia, madai na jinai lakini vile vile itahusisha huduma ya utoaji vyeti vya kuzaliwa.

"Tunataka watanzania wajue wakati umefika wa kupata msaada wa kisheria pasipo na malipo yeyote," alisema Balozi Chana.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka alitoa rai kwa wananchi mkoani hapa kujitokeza na kutumia fursa hiyo ambayo itasaidia kupunguza changamoto ya kuwaona viongozi mara kwa mara hasa kwenye masuala yanayohusu sheria.

"Samia Legal Aid inaenda kupunguza wingi wa watu wanaoenda kutoa malalamiko yao hasa kwenye ofisi za serikali, wananchi wengi wanaenda kwenye ofisi za wakuu wa wilaya na tunapofanya mikutano tunakutana na mambo mengi ambayo unaona yanamsingi wa kisheria na yanahitaji yapate majibu," alisema Mtaka.

Alisema kwenye Mkoa wa Njombe bado matukio ya visasi ni mengi na wengi wao hawaendi sehemu sahihi za kisheria sambamba na wakati wa ajira zinapotangazwa kumekuwa na foleni kubwa ya wananchi kulalamika kuhusu vitambulisho vya utaifa na vyeti vya kuzaliwa.

Nipashe ilizungumza na Mwenyekiti wa Mtaa wa Kambarage Njombe Mjini, France Msanga alisema kampeni hiyo itakuwa msaada mkubwa kwa wananchi kwani Njombe kumekuwa na wimbi kubwa la ukatili wa kijinsia, migogoro ya ndoa, ardhi pamoja na mauaji.

"Msaada wa kisheria umefika wakati sahihi kwa sababu mimi mtaa wangu una watu wengi sana lakini kesi nyingi sana ninazozisuluhisha kama mwenyekiti kesi za ndoa kwa sababu watu wanazaa watoto wanawatelekezea kinamama ambao wanaangaika peke yao katika malezi," alisema Msanga.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii Tanzania (SMAUJATA) Mkoa wa Njombe, Given Mtweve alikiri kuwapo kwa vitendo vya ukatili ambavyo vinapaswa kutokomezwa kwa njia ya wananchi kuungana ili kuvipinga.

## Wananchi walalamika kuchapwa viboko na viongozi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANANCHI wa Kata ya Kidegembye Halmashauri ya Wilaya ya Njombe Mkoa wa Njombe wamelalamikia vitendo vinavyofanywa na baadhi ya viongozi wa kata hiyo ikiwemo kuwachapa viboko pindi wanapofanya makosa.

Malalamiko hayo yalitolewa juzi kwenye mkutano wa Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilayani Njombe uliofanyika katika kata hiyo.

Walisema imefika wakati baadhi ya viongozi hao wamekuwa wakiwachapa viboko na kuwatoza faini kubwa kinyume cha sheria, jambo ambalo wameiomba serikali kulifanyia uchunguzi kwa haraka ili kuwasaidia.

Wananchi katika mkutano huo, Luka Mangua alisema lipo tatizo la baadhi ya wananchi kuchapwa viboko hadi kulazwa hospitali bila ya kufanya kosa lolote.

"Wanaacha kukamata wezi mitaani wanaenda kumkamata mtu kumvamia auze mali zake ili alipe faini kwa kosa ambalo hajalifanya," alisema Mangua.

Naye Beatrice Msigwa aliiomba serikali kuingilia kati kwa sababu unyanyasaji katika kata hiyo umezidi.

Alisema: "Pia tunaiomba serikali kuja kuwapatia elimu ili tuweze kujua na kuzitambua haki zetu za msingi kama raia katika jamii," alisema Msigwa.

Baada ya kusikilza kero za wananchi hao, Katibu wa Siasa na Uenezi Wilaya ya Njombe, Hhitler Msolwa alisema hatua za kidhamu zinaenda kuchukuliwa baada ya kupokea malalamiko hayo.



Mkuu wa Wilaya ya Rombo, mkoani Kilimanjaro, Raymond Mwangwala akipanda mti wakati wa kampeni ya upandaji miti kwenye hifadhi ya taifa ya Mlima Kilimanjaro, katika eneo la kijiji cha Mengeni Kitasha, juzi. PICHA: **MPIGAPICHA WETU**

## Watu sita mbaroni tuhuma mauaji

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

JESHI la Polisi Mkoa wa Njombe linawashikilia watu sita wakazi wa Kijiji cha Igosi wilayani Wanging'ombe kwa tuhuma za mauaji ya Onesmo Msigala (58) kwa kuhusishwa na imani za kishirikina.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi, Mahamoud Banga aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari mkoani hapa.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Jesca Kombo (34), Daud Msigala (28), Elia Mbwilo (16), Ben Msigala (16), Jimson Msigala (39) na Zakayo Muro (49).

Alisema watuhumiwa hao wanadaiwa kumuua mtu huyo kwa kumtuhumu kuwa amemuua mtoto wake ambaye tayari amezikwa Mei Mosi mwaka huu.

Kamanda Banga alisema mashtaka yanaendelea na watafikishwa mahakamani pindi upelelezi wa kesi utakapokuwa umekamilika.

Wakati huo huo, Jeshi la Polisi pia linamshikilia Amani Mdindile (14) mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Kitandililo kwa kosa la kumuua mtoto wa miaka mitatu.

Alisema pia, Jeshi la Polisi linawashikilia Athumani Yahaya (45) mkazi wa Dar es Salaam na Neema Kasanga (32) mkazi wa Wikichi mkoani Njombe kwa kuendesha shughuli za uganga bila ya kibali.

Aidha, alisema katika kipindi cha April mwaka huu Jeshi la Polisi limewakamata madereva 5,169 kwa makosa mbalimbali.

Kamanda Banga aliwataka wananchi kuzingatia sheria za usalama barabarani na kuendelea kushirikiana na jeshi hilo kwa kuwafichua wahalifu na kuacha kuwafanyia vitendo vya unyanyasaji watoto wadogo.

Aidha, alitoa wito kwa wakazi wa Mkoa wa Njombe kuachana na imani za kishirikina, uhalifu kwani hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa wale wote watakaovunja sheria.

Pia, aliwataka wazazi kuwa karibu na watoto wao kwakuwa mkoani Njombe matukio mengi ya kikatili hutendwa na wanafamilia wenyewe.



## Ukuaji wa miji chanzo kutokea umeme mdogo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Maji, Nishati na Madini imesema kutokana na kuongezeka kwa miji mipya na ukuaji wa matumizi ya umeme, baadhi ya maeneo yanakumbwa na tatizo la umeme mdogo.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Mtambwe, Dk. Mohamed Ali Suleiman aliyetaka kujua mbinu za serikali katika kuhakikisha ubora na usalama wa mita za umeme kabla ya kufungwa kwa mtumiaji wa mwisho.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Zawadi Amour alisema inapotokea hali ya umeme mdogo mita haiwezi kuhimili kufanya kazi kama kawaida na kusababisha kuzima wakati wa matumizi ya juu hususani nyakati za usiku

Alisema kutokana na hali hiyo inasababisha wananchi kulalamika kuhusu uwepo wa umeme mdogo.

"Nipende kuwahakikishia mita zetu zote zina ubora na zipo salama kwa watumiaji, vile vile Shirika la Umeme Zanzibar kila linapogundua eneo limeanza kupata umeme mdogo kutokana na ukuaji wa miji, linaongeza line nyingine na kuweka transformer ili kuondoa tatizo la umeme mdogo na mita kuzima na kuwaka" alisema.

Alisema mbinu ambayo inatumika ni kuhakikisha mita zinazofungwa zimefikia vigezo vilivyowekwa na vile vile kuhakikisha mita zote kabla hazijapokelewa ghalani zinapimwa katika 'Test Bench' iliopo katika lebo ya Shirika la Umeme kabla kuifunga kwa mtumiaji.

Alisema: "Mheshimiwa Spika, wastani wa mita zinazoingia katika Shirika la Umeme Zanzibar kwa mwaka ni pisi 43, 000 na wastani wa mapato yanayokusanywa na shirika kwa mwaka ni Sh. bilioni 4.8".

Naibu waziri huyo pia alikiri kuwa Taasisi ya Wakala wa Vipimo Zanzibar (ZAWEMA) haikuwa yenye kushirikishwa kuhusu suala la upimaji wa mita zinazoingizwa.

Alisema hali hiyo inatokana na shirika halikua na uelewa wa kutosha na taasisi hiyo mpya ambayo kisheria imeanza kufanya kazi rasmi kwa Sheria ya Mwaka 2020.

Hata hivyo, alisema tayari wameanza kufanya mazungumzo na Wakala wa Vipimo Zanzibar ambapo wanatarajia kuanza kushirikiana.

**Mheshimiwa Spika, wastani wa mita zinazoingia katika Shirika la Umeme Zanzibar kwa mwaka ni pisi 43, 000 na wastani wa mapato yanayokusanywa na shirika kwa mwaka ni Sh. bilioni 4.8.**

# Serikali yahimiza uboreshaji sekta ya usafiri wa anga

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed, amesema, sekta ya usafiri na usafirishaji angani ni muhimu katika dunia ya sasa, kwamba asilimia 30 ya mizigo yote inatumia usafiri huo.

Aliyasema hayo juzi wakati akifungua mkutano wa wadau wa nchi 40 za Afrika katika masuala ya usafiri wa anga hasa katika ndege za mizigo uliofanyika visiwani Zanzibar.

Alisema usafiri huo umekuwa ni njia inayotumika sana hasa dunia inapopata majanga, kwamba mahitaji mengi ya binadamu yanahitajika na usafiri unaotumika ni wa ndege za mizigo.

Aidha, alisema kuna umuhimu wa kuwapatia mafunzo watendaji hao ili kutoa fursa kwa wanachama wa nchi za Afrika kubadilishana uzoefu na fikra kwa lengo la kuja na mikakati ya kupunguza ama kuondosha athari zinazoweza kuondosha ajali zitakazosababisha maafa kwa watu na upotevu wa mali.

Hivyo, alisema kuwepo kwa mafunzo hayo yatasaidia kuangalia usalama na inawezekana ndege hizo zikatumika kuficha vitu vya hatari ikiwemo milipuko, usafirishaji wa dawa za kulevya.

"Njia hii inaonekana ni ya haraka sana, pia ni rahisi kuingiza kwa njia nyingine lakini ni salama kama haitoingiliwa na watu wanaopenda kufanya uhalifu" alisema.

Sambamba na hayo, alisema kuna haja ya kupeana mikakati madhubuti utakaosaidia nchi hizo kuweza kuongeza viwango vya usafirishaji vinavyoendana na hali iliyopo hivi sasa.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TCAA), Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti wa Shughuli za Usalama wa Anga Tanzania, Salim Ramadhan Msangi, alisema, mkutano huo utazungumzia usalama wa eneo la mizigo inayosafirishwa ambapo eneo hilo magaidi wanalitumia kushambulia ndege za mizigo na abiria.

Alisema, wanalenga sana ndege hizo kwasababu huwa na mizigo mikubwa, hivyo kuwepo kwa mafunzo hayo ni kubadilishana uzoefu wa kazi katika nchi zao sambamba na kupata mafunzo ya namna ya kudhibiti na kuzuwia uhalifu kwa nchi za Afrika hasa kwa usafiri wa anga.

Naye, Mkurugenzi Mkuu wa ZAA, Seif Abdallah Juma, alisema matarajio ya mkutano huo kuendelea kufanya vizuri katika uingizaji wa mizigo na katika kiwango kilichokuwa bora katika utoaji wa huduma.

Hivyo, aliahidi kuendelea kufanya kazi zilizokuwa na kiwango cha hali ya juu ili kuona hali ya usalama wa anga na usafirishaji unakuwepo katika kiwanja chao.



Kaimu Mganga Mkuu wa Hospitali ya CCBRT, Dk. Francis Mchomvu (katikati), akikata keki pamoja na mmoja wa akinamama wanaopatiwa matibabu ya fistula hospitalini hapo, Dar es Salaam jana, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimaitaifa ya kutokomeza ugonjwa wa Fistula. Kushoto ni Mkuu wa Idara ya Afya ya Uzazi na magonjwa ya akinamama wa hospitali hiyo, Dk. Daniel Michael. **PICHA: JOHN BADI**

# Shule 217 kuunganishwa na mkongo wa taifa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar imesema katika kutekeleza mageuzi makubwa ya elimu kidijitali shule 217 zinatarajiwa kuunganishwa na mkongo wa taifa kwa ajili ya kupata mawasiliano ya kisasa ya teknolojia ya TEHAMA.

Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Abdulgulam Hussein, aliyasema hayo wakati akijibu swali la mwakilishi wa jimbo la Mwanakwerekwe Ameir Abdalla Ameir, aliyetaka kujua hatua zilizofikiwa kwa sasa katika mageuzi makubwa ya elimu ya mtandao.

Gulam alisema jumla ya shule za sekondari 217 zinatarajiwa kuunganishwa na mkongo wa taifa wakati vituo vya ubunifu Hub 22 vitapata huduma za mawasiliano ya mtandao.

Aidha, alisema vituo vya mafunzo kwa walimu 10 vinatarajiwa kuunganishwa na huduma za mtandao wa kasi wa mawasiliano kwa ajili ya kuwawezesha walimu kutekeleza majukumu yao.

Alisema shule zote ziliopo katika visiwa vidogo zitaunganishwa na huduma za mawasiliano ya huduma za Intaneti kupitia mkongo wa taifa.

Alizitaja shule ziliopo katika visiwa vidogo ambavyo vitanufaika na huduma hiyo ikiwemo Kojani pamoja na Kisiwa cha Tumbatu ambapo shule za ghorofa zinajengwa kwa sasa.

"Mheshimiwa Spika nataka niwaambie wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba shule za sekondari 217 zitaunganishwa na huduma za mawasiliano ya intaneti ikiwa ni sehemu ya mageuzi makubwa ya sekta ya elimu"alisema.

Naibu waziri huyo alipongeza Benki ya Dunia (WB) ambayo inatekeleza miradi hiyo ya mageuzi makubwa katika shule za Unguja na Pemba kuingia katika mfumo wa kidijitali wa mawasiliano ya TEHAMA ambayo yatasaidia na kuongeza ufaulu wa wanafunzi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KISARAWE Kituo cha SUNGWI Mkoa PWANI Shauri la Madau No 07/z024**
**Jina la mdai HARIF NASIR AHAMED**
**Jina la mdaiwa ATHUMANI MATEI**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai katika Mahakama ya Mwanzo)**
**Kwa ATHUMANI MATEI**
**P.O.BOX 7201**
**BUGURUNI – DAR ES SALAAM**

**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yako kwamba**
Mdai ameleta madai ya pesa Tsh 23,500,000/= Milioni Ishirini na tatu na laki tano tu) dhidi ya mdaiwa kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 27 Mwezi 05 Mwaka 2024 saa 4.00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 16 Mwezi 05 Mwaka 2024.

Roelgers
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO

## KUPOTEA KWA VYETI



**GLADNESS MUNGAYA** anatangaza kupotelewa na vyeti,cha kidato cha nne chenye index namba S1864-0039 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya **KIRANYI** mwaka 2012 na cheti cha kurisiti(kurudia)kidato cha nne chenye index namba **P1110-0022** kupitia kituo/shule ya sekondari ya **KALOLENI** mwaka 2014,yeyote atakaye viokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **ARU/ARU/RB/440669/2019**

## KUPOTEA KWA CHETI



**GLADNESS MUNGAYA a**natangaza kupotelewa na cheti cha chuo cha **BASIC TECHNICIAN kozi ya CERTIFICATE OF COMMUNITY HEALTH** chenye namba ya usajili **NP1110/0022/2024** kilichotolewa na chuo cha A3 **INSTITUTE OF PROFFESIONAL STUDIES** mwaka **2017**, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Polisi taarifa ARU/ARU/RB/440669/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**VENA FANUEL SIMON** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S23360092** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **UBUNGO MODERN SECONDARY SCHOOL** mwaka **2010.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/75184/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALLEX JAMES NDYAMKAMA**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NO YA USAJILI **T966DQP**
CHASSIS NO: **KM510022306**
ENGINE NO: **5K0511254**
LITEACE TRUCK
YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI
**PHQ/ARU/ARU/16573/2024**.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU DODOMA**
**SHAURI LA MADAI NA. 4381 YA 2024**
**EMMANUEL TEMBA.......................................MDAI**
**DHIDI YA**
**SARA STEVEN.....................................MDAIWA**

**KWA: SARA STEVEN**
**POPOTE PALE ULIPO**

**YAH: TAARIFA YA KUTAJWA KWA SHAURI LA MADAI NA.4381 YA 2024**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA.**
**UNAFAHAMISHWA KWAMBA;** Shauri tajwa hapo juu litatajwa Mahakama kuu ya Tanzania Dodoma mbele ya **MHE. E. E. KAKOLAKI, JAJI** wa Mahakama kuu ya Tanzania Dodoma , saa tatu (3:10) asubuhi siku ya Jumanne tarehe 23/7/2024.
HIVYO; Unatakiwa Ufike wewe wenyewe au Wakili wako siku hiyo iliyotajwa bila kukosa .
**NA ENDAPO;** Hutofika wewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itakanyoamua pasipo wewe au wakili wako kuwepo.
**IMETOLEWA;** Kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama leo hii tarehe 22/05/2024.

NAIBU MSAJILI
DODOMA

**IN THE COURT OF DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause No 9616 OF 2024**
**IN THE MATTER of the estate of the late**
**SAMWEL NATHANIEL SAMSON**
**And**
**IN THE MATTER of Application for letters of administration by**
**NATHANIEL SAMSONI MKWALILA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN NO. 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on before the 11 day of 6...2024
**Dated at DODOMA 21 day of 5......2024.**

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**SULEIMAN MATHEW IKOMBA** anatangaza kupotelewa na hati ya kusafiria yenye namba **TAE589838** iliyotolewa na wizara ya mambo ya ndani ya nchi **(UHAMIAJI) DAR ES SALAAM** mwaka 2023, yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Polisi taarifa PHQ/DAR/TEM/94371/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**DHAMOTHARAN BALAKRISHAN** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya BAJAJ BOXER yenye namba za usajili MC121 DMJ, yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa
**PHQ/PWA/KIB/8558/2024**


**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**
**Piga Simu 0677020701**

**KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTE KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 - 0677020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**

**OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industrial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 0677020701**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**Website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Mataifa 50 kukutana Uswisi kujadili amani Ukraine, Russia

**BERN, Switzerland**

USWISI inaratajia kuwaalika washiriki zaidi ya 160 kutoka mataifa mbalimbali katika mkutano utakaolenga kuleta amani na upatanishi wa Ukraine na Russia.

Mkutano huo unatarajiwa kufanyika kwa siku mbili kuanzia Juni 15 hadi 16 katika Hoteli ya Burgenstock Hotel nchini humo.

Taarifa iliyotolewa na Idara ya Mamlaka ya Mambo ya Nje ya Uswisi ilieleza kuwa waalikwa hao ni wanachama kutoka mataifa saba yenye nguvu kubwa ya uchumi ya G7, G20, Umoja wa Ulaya (EU) Nchi wanachama wa Brics isipokuwa Russia.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, waalikwa wengine ni mashirika mbambali ya kimataifa na kidini.

"Hii itakuwa ni jitihada za tano kunurusu hali ya amani kati ya Russia na Ukraine. Wageni watatoka pia mataifa ya Afrika Kusini, Misri, Senegal, Congo-Brazzaville, Comoro, Zambia na Uganda ambao wataongozwa na Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa," ilieleza taarifa hiyo.

Kadhalika, ilieleza kwamba wiki iliyopita, redio ya kijamii ya Uswisi, RTS ilitangaza zaidi ya mataifa 50 yamethibitisha kushiriki mkutano huo.

Ilieleza kuwa baadhi ya washiriki ni Rais wa Kamisheni ya Ulaya, Ursula von der Leyen na Rais wa Baraza la Ulaya, Charles Michel.

Wengine ni Kansela wa Ujerumani, Olaf Scholz, Kiongozi wa Serikali ya Italia, Giorgia Meloni, Waziri Mkuu wa Canada, Justin Trudeau pamoja na Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa mkutano wa kwanza wa kujadili amani Ukraine ulifanyika Juni 2023 katika mji wa Copenhagen, wa pili ulifanyika Agosti, 2023 mjini Jeddah Saudia Arabia ukiwajumulisha wakishiriki kutoka mataifa 40 ikiwamo China, India, Brazil, Afrika Kusini, Indonesia, Mexico, Zambia, Misri na Marekani.

Ilieleza kuwa mkutano wa tatu ulifanyika Oktoba, 2023 Malta ukishirikisha mataifa 65 kutoka Ulaya, Amerika ya Kusini, Uarabuni, Afrika na Asia.

Mwenyekiti wa mkutano huo, Waziri wa Mambo ya Nje wa Uswisi, Ignazio Cassis, alisema: "Mkutano utakuwa na masuala mbalimbali ya kujadili. Hadi sasa siyo Ukraine wala Russia waliokubali kuachia eneo. Ndiyo sababu Rais wa Uswisi, Viola Amherd ameitisha mkutano huo wa kutafuta amani".

Ikieleza sababu za Afrika kuhudhuria mkutano huo, Ignazio alisema mgogoro huo umesababisha madhara makubwa ya kiuchumi ikiwemo uhaba wa nafaka na mbolea, hali iliyosababisha kupaa kwa bei ya vyakula katika nchi nyingi.

*SWIS NEWS*



Maelfu ya raia wa Iran wakizuia gari lililobeba jeneza la Rais wa Iran, Ebrahim Raisi wakati likielekea eneo la makaburi jana. **PICHA: REUTERS**

IRAN YASIMAMA

# Maelfu wazuia jeneza barabarani, biashara, huduma zasitishwa

**TEHRAN, Iran**

MAISHA yamesimama kwa siku nzima ya jana, wakati mwili wa Rais wa Iran, hayati Ebrahim Raisi, ukipelekwa eneo la makaburi ya nyumbani kwake Mashad.

Dua na vilio vilitawala wakati maelfu ya waombolezaji walipojitokeza katika barabara kuu inayoelekea katika eneo takatifu la Imam Reza na kusababisha gari lililobeba jeneza la kiongozi huyo na viongozi wengine saba kukwamishwa na msongamano.

Raisi alifariki Jumapili iliyopita kwa ajali ya helikopta kwa kile kilichoelezwa ni hali mbaya ya hewa.

Waombolezaji hao wengi wao wakiwa wamevaa nguo nyeusi na kubeba bendera nyeusi, walitanda katika barabara kuu ya mji huo. Hali ya jua kali haikutatiza wananchi wa Iran kujitokeza kwa wingi kuulaki na kuuzika mwili wa kiongozi huyo aliyekuwa namba mbili kwa madaraka na umaarufu kutokana na misimamo yake mikali.

Baadhi ya waombolezaji waliofanikiwa kulifikia gari hilo, walionekana wakiwapa askari vitambaa vyao kwa ajili ya kutoa baraka kwa marehemu, huku wengine wakibubujikwa na machozi ya uchungu.

Rais Raisi na watu wengine saba akiwemo waziri wake wa mambo ya kigeni, Hossein Amirabdollahian walifariki katika ajali hiyo iliyotokea karibu na mpaka wa nchi ya Azerbaijan.

## Wapalestina 35 wauawa Rafah

**GAZA, Palestina**

VIKOSI vya Israel vimeendelea kufanya mashambulizi katika mji wa Rafah, na usiku wa kuamkia jana Wapalestina 35 wameripotiwa kuuwawa.

Hata hivyo, vikosi vya askari wa ardhini vimeonekana kusonga mbele katika maeneo ya pembezoni mwa mji huo ambao una idadi kubwa ya watu.

Serikali ya Israel ilisema haina chaguo lingine bali kuushambulia mji huo kwa lengo la kuwamaliza wapiganaji wa Hamas ambao inaamini wamejificha ndani ya mji huo.

Wanajeshi walikuwa wakiingia polepole ndani ya viunga vya mashariki mwa Rafah tangu mwanzoni wa mwezi Mei

Wakati jeshi la Israel likiendelea na operesheni zake, bado lilisema liko tayari kuanzisha tena mazungumzo yaliyokwama juu ya kupata makubaliano ya kusitisha mapigano na kuwaachilia mateka wanaoshikiliwa na Hamas.

Shinikizo la kimataifa la kusitisha mapigano limeongezeka kwa Israel na Waziri Mkuu wa nchi hiyo, Benjamin Netanyahu, amezidi kubanwa kutokana na nchi tatu za Ulaya kutangaza kutambau taifa la Palestina.

*DW*

## China yafanya mazoezi kijeshi kuzunguka Taiwan

**BEIJING, China**

KATIKA kuonyesha nguvu yake ya kijeshi, China imeanza mazoezi ya kuzunguka Taiwan baada ya tukio la Rais mpya wa kisiwa hicho, William Lai kuapishwa siku nne zilizopita.

Msemaji wa jeshi la ukombozi wa watu wa China, Li Xi, ameltaja tukio hilo sawa na kuonyesha adhabu kali kwa kiongozi huyo kutaka kujitenga.

Mazoezi hayo, yaliyoanza mapema Alhamisi, yanafanyika kuzunguka kisiwa hicho ikiwa ni pamoja na Mlango wa bahari wa Taiwan kuelekea magharibi yake, na kuzunguka visiwa vinavyodhibitiwa na Taiwan vya Kinmen, Matsu, Wuqiu na Dongyin. Wizara ya Ulinzi ya Taiwan ililaani vitendo hivyo vya China na kuvitaja kuwa ni uchochezi.

Taarifa hiyo ilisema nchi hiyo imetuma vikosi vya majini, anga na ardhini kwa ajili ya kutetea mamlaka ya kisiwa hicho.

Jeshi la China limesema mazoezi yake yanalenga doria za pamoja za utayari wa kupambana na anga, mashambulizi ya usahihi katika malengo muhimu, na operesheni jumuishi ndani na nje ya kisiwa hicho ili kupima uwezo wa pamoja wa kupambana na vikosi vyake.

*BBC*

Wachezaji wa Azam FC wakishangilia baada ya kufunga bao katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya JKT Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamhuyo, Dar es Salaam juzi. Azam FC ilishinda mabao 2-0. PICHA: MTANDAO




# KMC YAKUBALI KWENDA ARUSHA

**Na Saada Akida**

MECHI ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Simba dhidi ya KMC FC itachezwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini, Arusha, imefahamika.

Ofisa Habari wa Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB) , Kareem Boimanda, amesema mechi hiyo haitachezwa kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo ulioko Mbweni, Dar es Salaam.

Boimanda amesema TPLB ina haki na jukumu la kuchagua uwanja au kituo cha kuchezwa mechi na timu zinalazimika fuata maelekezo ya kufika kwenye sehemu husika waliyopangiwa.

Ofisa huyo alisema tayari timu zote zimepewa taarifa kuhusiana na uwanja rasmi utakaotumika kwa ajili ya mechi hiyo na wanatakiwa kufuata mwongozo huo.

"Hii mechi itachezwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha na sio Meja Isamuhyo, hakuna timu ambayo itaweza kugomea uwanja au kituo kilichochaguliwa na Bodi au Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF)," alisema Boimanda.

Naye Ofisa Habari wa KMC FC, Khalid Chukuchuku, amesema baada ya kikao cha pande zote tatu, uongozi wa timu hiyo umekubali kuelekea Arusha kwa ajili ya kucheza mchezo huo.

„Awali mechi ilikuwa Meja Jenerali Isamuhyo, tulijua hivyo lakini baada ya kikao hicho tumekubaliana na Bodi na sasa tunaanza safari ya kwenda Arusha kwa ajili ya mchezo wetu dhidi ya Simba," alisema Khalid.

Simba iko katika vita ya kuwania nafasi ya pili ikichuana na Azam FC, kila moja ikiwa na pointi 63 kibindoni.

## Adam, Mashujaa waagana, Azam FC yamtolea 'macho'

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Mashujaa FC inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara imetangaza rasmi kuachana na straika wake, Adam Adam, bila kuweka wazi sababu zilizopelekea uamuzi huo, taarifa za ndani zinasema nyota huyo anawindwa na Azam FC.

Taarifa iliyotolewa na Mashujaa FC jana inasema uamuzi huo umefikiwa baada ya kufikiwa kwa makubaliano ya pande zote mbili.

Idara ya Habari na Mawasiliano ya Mashujaa imemtakia kila la kheri katika safari yake mpya kwenye mchezo huo wa soka.

„Klabu ya Mashujaa FC inapenda kuutaarifu umma tumeachana na mchezaji, Adam Omary Adam, kwa makubaliano ya pande zote mbili. Hatua hiyo ya kuachana na nyota huyo imefikiwa baada ya makubaliano ya pande zote mbili na uongozi unamtakia kila la kheri katika safari yake ya mchezo wa soka," ilisema taarifa hiyo.

Taarifa zilizopatikana jijini, Dar es Salaam zinasema straika huyo mwenye mabao saba msimu huu anawaniwa na Azam FC, ambayo imeanza kujipanga kuimarisha kikosi chake kwa ajili ya msimu ujao wa mashindano mbalimbali watakayoshiriki.

Kabla ya kutua Mashujaa FC, straika huyo ameshazichezea klabu kadhaa za Ligi Kuu Bara ikiwamo JKT Ruvu, Polisi Tanzania na Mtibwa Sugar, lakini pia aliwahi kwenda kucheza soka la kulipwa nchini Libya katika klabu ya Al Wahda Tripoli.

## Singida FG yaipigia hesabu Geita Gold

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha Singida Fountain Gate kimesema kiko tayari kwa ajili ya kusaka pointi tatu muhimu watakapoikabili Geita Gold katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Ngawina Ngawina, alisema wachezaji wana morali ya juu kuelekea mchezo huo na anaamini watazibakisha pointi tatu nyumbani.

„Malengo yetu ni kupata pointi tatu katika mchezo huo ambao unatarajiwa kuwa na upinzani mkubwa, kila mchezaji ana ari ya ushindi,' alisema Ngawina.

Aliongeza hana wasiwasi na mchezo huo kutokana na maandalizi mazuri waliyofanya na wamejiandaa kuingia kwa tahadhari licha ya wapinzani wao kupata kichapo cha mabao 4-1 kutoka kwa Simba.

„Tunajua hauwakuwa mchezo rahisi kwa sababu Geita Gold pia wako katika hatari ya kushuka daraja, tunafahamu wataingia kucheza kwa nguvu ili kusapa ushindi utakaowanusuru na janga la kushuka daraja," Ngawina alisema.

## Mwadui FC yapanda, Copco yaporomoka

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Mwadui FC imefanikiwa kupanda daraja kucheza Ligi ya Championship baada ya kulazimisha sare ya mabao 2-2 dhidi ya Copco katika mechi ya ‚play off', iliyochezwa kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini, Mwanza juzi.

Mwadui imepanda daraja baada ya kupata ushindi wa jumla ya mabao 5-2, ikishinda mabao 3-0 katika mechi ya kwanza iliyochezwa Mei 17, mwaka huu kwenye Uwanja wa Nyankumbu, Geita.

Copco ikishuka, Green Warriors imebaki katika Ligi ya Championship, baada ya kuichapa Malimao FC mabao 2-1 mechi nyingine ya mchujo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Mbweni, juzi.

Timu hiyo imesalimia kwa ushindi wa jumla wa mabao 4-1, mechi ya kwanza iliyochezwa kwenye Uwanja wa Kituo cha TFF, Kigamboni ilishinda mabao 2-0.

Baada ya kipigo hicho, Malimao FC, yenye maskani yake mkoani Katavi, ineshindwa kupanda na sasa msimu ujao itashiriki tena ‚First League' maarufu Ligi Daraja la Pili huku Pan African na Ruvu Shooting zimeshuka moja kwa moja.

## ZISIKUPITE

### JASON KUPUNGUZIWA
KLABU ya Manchester United wanataka takriban asilimia 75 ya pauni milioni 75 walizolipa Borussia Dortmund kwa winga wa Uingereza, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 24, ambaye atahitaji kupunguzwa mshahara wake wa pauni 275,000 kwa wiki ikiwa klabu hiyo ya Bundesliga itakamilisha dili la kumsaini tena ***(Sun)***

### RB YAMBANA SESKO
RB Leipzig wamempa mshambuliaji wa Slovenia, Benjamin Sesko mwenye umri wa miaka 20, ambaye anahusishwa na kuhamia Arsenal nyongeza ya muda wa mkataba wa mwaka mmoja. ***(Fabrizio Romano)***

### LOMMEL YAMTAZAMA SOUZA
KLABU ya Sheffield United ingelazimika kulipa kiasi cha tarakimu sita kwa kiungo wa kati wa Brazil, Vinicius Souza, kwa timu yake ya zamani ya Lommel iwapo mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 angeanza katika mechi dhidi ya Tottenham Hotspur. ***(Sun)***

### TEN HAG ATAJWA BAYERN
BEYERN Munich na Ajax wanaendelea kupigania sahihi ya Erik ten Hag mwenye umri wa miaka 54, kwa imani atafutwa kazi kama Kocha Mkuu wa Manchester United mwishoni mwa msimu huu. ***(Mirror)***

### RAYA, ARSENAL HAKIJAELEWEKA
KIPA wa Hispania, David Raya, mwenye umri wa miaka 28 amesema hajafanya mazungumzo yoyote na Arsenal kuhusu iwapo watafanya uhamisho wake wa mkopo kutoka Brentford kuwa wa kudumu. ***(Express)***

### ANGE KUSAJILI MASTRAIKA
KOCHA wa Tottenham Hotspur, Ange Postecoglou, ataweka kipaumbele kumsajili mshambuliaji mpya na kiungo wa safu ya ulinzi huku akipanga kuwaachilia wachezaji wengi msimu wa joto ***(Mirror)***

### ISWICH KUMBAKIZA MCKENNA
KLABU ya Iswich inasema wanafanya kila linalowezekana kuhakikisha Kocha, Kieran McKenna, anasalia katika timu yao huku kukiwa Brighton, Chelsea na Manchester United zikitajwa pia kumwania mwalimu huyo. ***(Teamtalk)***

### ARSENAL YATAKA UBINGWA
MWENYEKITI mwenza wa Arsenal, Josh Kroenke, amewaambia mashabiki "klabu haitasimama tuli" inapotafuta wachezaji ili kusaidia kupata taji la Ligi Kuu England na Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Goal)***

### BROWN KUTUA WEST HAM
KLABU ya West Ham wanakaribia kumsajili mlinzi mwenye umri wa miaka 18 ambaye ni raia wa England, Luis Brown, kutoka Arsenal. ***(Caught Offside)***

### COADY SOKONI ENGLAND
KLABU ya Stoke City imeonyesha nia ya kutaka kumsajili beki, Conor Coady, mwenye umri wa miaka 31 kutoka Leicester ***(Teamtalk).***

### KONATE AGEUKA LULU
LEICESTER inajiandaa kushindana na klabu za Ufaransa Lyon na Brest kumnunua fowadi wa Burkina Faso, Mohamed Konate, mwenye umri wa miaka 26, ambaye mkataba wake na Akhmat Grozny ya Urusi utamalizika msimu huu. ***(Football Insider)***

## DOND... OKA MAGAZ... LAYA



# KOMPANY ANUKIA BAYERN MUNICH

Vigogo hao wa Ujerumani wanajiandaa kuilipa Burnley dau la...

**MUNICH, Ujerumani**

BAYERN Munich imepotiwa kukaribia kuafikiana na Vincent Kompany ili kuwa kocha mkuu mpya wa timu hiyo.

Kompany amefanya vyema katika Ligi Kuu England msimu huu, licha ya kushindwa kubaki na klabu ya Burnley ambayo yeye mwenyewe aliipandisha daraja mwaka mmoja uliopita, na mazungumzo na Bayern Munich yalianza wiki hii.

Gazeti la The Guardian linaandika kwamba mazungumzo hayo yamefikia "hatua ya juu" na kwamba Bayern wanawasiliana na Burnley kuhusu kiasi cha fidia kitakacholipwa.

Bayern Munich wamekataliwa mara nyingi tangu walipoamua kuachana na Thomas Tuchel. Uamuzi huo ulifanywa hapo awali mnamo Februari, na Mjerumani huyo aliona nje msimu badala ya kurudia kampeni ya awali wakati Julian Nagelsmann alifukuzwa mapema Machi.

Lakini Xabi Alonso alisalia kuwa mwaminifu kwa Bayer Leverkusen, Nagelsmann aliongeza muda wa kuinoa Timu ya Taifa Ujerumani na Ralf Rangnick pia alisema hapana.

Kulikuwa na jaribio fupi la kutaka kumbakisha Tuchel, lakini hakutaka kubaki.

Kompany mwenye umri wa miaka 38, ingawa mgombea mshangao kutokana na ukosefu wake wa uzoefu wa usimamizi, ana sifa nyingi.

Alikuwa mchezaji mwenye akili, amesifiwa kwa mbinu zake, na alikuwa anajua mbinu za Pep Guardiola kwa miaka mitatu akiwa Manchester City.

Ustadi wa kujua Kijerumani, ingawa sio lazima kabisa na Kompany anazungumza kwa ufasaha, alitumia wakati wake akicheza huko Hamburg.

Bayern wataanza msimu wa 2024/25 wakitafuta kutwaa taji la Bundesliga kutoka kwa Bayer Leverkusen.

# LEWANDOWSKI: SIONDOKI BARCELONA

●●● Amesema atasalia katika kikosi hicho cha timu hiyo inayoshiriki LaLiga kwa ajili ya msimu ujao na watashinda...



**BARCELONA,** HISPANIA

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Robert Lewandowski, amesema atasalia katika kikosi hicho cha timu hiyo inayoshiriki LaLiga kwa ajili ya msimu ujao na watashinda „mataji mengi“ mbeleni.

Lewandowski, ambaye alijiunga na Barca kutoka Bayern Munich mwaka 2022, amefunga mabao 58 katika michezo 94 kwenye mashindano yote tangu kuwasili kwake.

Alikuwa muhimu katika kuwasaidia kushinda taji lao la kwanza la ligi tangu mwaka 2019 na Kombe la Super Cup la Hispania msimu wa 2022-23.

Licha ya kampeni isiyo na taji mwaka huu, Lewandowski ameonyesha nia ya kusalia Barca na ana imani wanaweza kushinda taji msimu ujao.

"Kwa kweli, kwangu ni wazi sana. Nataka kushinda mataji mengi nikiwa na Barcelona na nina uhakika msimu ujao tutakuwa na nguvu zaidi na pia tutashinda mataji,“ alisema Lewandowski akiliambia Mundo Deportivo alipoulizwa kuhusu uvumi wa kuwa ataondoka.

"Siku zote nataka kilicho bora sio kwangu tu, bali kwa wachezaji wenzangu na nina uhakika timu hii itashinda mataji msimu ujao kwa sababu naona tunachofanya kila siku, kwangu hilo ndilo muhimu kwa sababu hii ni klabu ambayo naishikilia karibu na moyo wangu na ninataka kutoa mengi kwa ajili ya timu.“

**Msimu wa Barcelona umetawaliwa na hali ya sintofahamu inayomzunguka Kocha, Xavi Hernández, pamoja na masuala ya kifedha ambayo klabu hiyo inakabiliana nayo, huku kukiwa na mapendekezo kwamba wanaweza kulazimika kuwaondoa wachezaji ili kupunguza matatizo yao.**

Kumekuwa na uvumi Lewandowski, ambaye alikuwa mshindi wa tuzo ya Ballon d'Or mwaka 2021, anaweza kuwa mmoja wa wachezaji hao, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35 amesema anataka kusalia katika klabu hiyo.

Barcelona watamenyana na Sevilla katika mchezo wao wa mwisho wa msimu utakaochezwa keshokutwa baada ya hapo Rais, Joan Laporta atakutana na Xavi kujadili mustakabali wa kocha huyo.

## Ederson kuondoka Man City

**MANCHESTER,** ENGLAND



GOLIKIPA wa Manchester City, Eder-Santana de Moraes, anatajwa kuwa mbioni kuihama klabu hiyo, yomsajili miaka saba iliyopita.

Taarifa zilizochapishwa katika Gazeti la The Mirror mapema meeleza mlinda mlanhuyo kutoka Brazil anajipanga kuondoka na kutimkia Saudi Arabia.

Ederson mwenye umri wa miaka 30 alijiunga na City kutoka Benfica mwaka wa 2017, na kushinda mataji sita ya Ligi Kuu England, Ligi ya Mabingwa Ulaya na mataji mawili ya FA.

Gazeti hilo liliandika: "Ederson anaweza kuwa mmoja wa wachezaji wa hadhi ya juu zaidi kuondoka kwenye kikosi cha Pep Guardiola katika kipindi hiki cha usajili wa majira ya kiangazi.“

Mashabiki wa City wanahofia huenda mlinda mlango huyo chaguo la kwanza akawa tayari kuondoka baada ya miaka saba klabuni hapo, huku Ligi Kuu ya Saudia ikitajwa kumtwaa.

Ingawa Man City hawataki kumwachia Ederson, lakini endapo itapokea ofa kubwa huenda ikamruhusu.

## Chelsea yasaka kocha mpya

**LONDON,** ENGLAND

THOMAS Frank wa Brentford na Vincent Kompany wa Burnley, majina yao yamekuwa ya kwanza kutajwa katika mpango wa kurithi nafasi ya Mauricio Pochettino ambaye ataondoka Chelsea.

Mabosi wa Chelsea wametangaza kuachana na Pochettino kwa makubaliano ya pande zote mbili ya kuvunja mkataba ambao ulisainiwa mapema msimu wa 2023/24.

Kocha huyo alisaini mkataba wa miaka miwili, hivyo sehemu ya mwaka mmoja katika mkataba wake ndio imevunjwa kwa makubaliano maalum yaliyofikia kati yake na uongozi wa juu wa Chelsea.

Taarifa iliyochapishwa na Gazeti la The Guardian imeeleza uongozi wa Chelsea umeanza kujipanga katika mchakato wa kumsaka kocha mpya, huku ukiamini Frank wa Brentford na Kompany wa Burnley watapata upinzani kutoka kwa makocha wengine watakaopendekezwa kurithi mikoba ya Pochettino

Aidha, Gazeti la The Telegraph limeongeza Kocha wa Stuttgart, Sebastian Hoeness, Michel wa Girona, Kieran McKenna wa Ipswich na Enzo Maresca wa Leicester wataingizwa katika kinyang'anyiro hicho.

HABARI MICHEZO

# MAKUSU ATAJWA KUMRITHI JOBE MSIMBAZI 2024/25

**Na Adam Fungamwango**

WEKUNDU wa Msimbazi wanatajwa wako katika mipango ya kumsajili straika, Jean-Marc Makusu Mundele, kutoka DC Motemba Pembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), imefahamika.

Hii ni mara ya pili kwa Simba kufanya mchakato wa kumsajili straika huyo ambaye ni raia wa DRC, baada ya kushindwa kukamilisha dili hilo msimu uliopita.

Straika huyo wa zamani wa Klabu za AS Vita, St. Eloi Lupopo na Orlando Pirates ya Afrika Kusini, kwa sasa anaichezea Hajer FC ya Saudi Arabia.

Habari kutoka ndani ya Simba zinasema straika huyo anaweza kutua kuchukua nafasi ya mshambuliaji, Pa Omari Jobe, ambaye huenda akaachwa mara baada ya msimu huu kumalizika.


Naye Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amesema wameamua kuipeleka Arusha mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC kutokana na sababu za ‚kimkakati' licha ya awali kuomba ichezwe kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo.

„Kuna sababu mbili au tatu kubwa kubwa zilizotufanya tuipeleke mechi Arusha, kwanza kabisa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid umekuwa na bahati kubwa sana kwetu, kwani mara ya mwisho katika mechi ya Ligi Kuu kwenye uwanja huo tuliifunga Coastal Union mabao 7-0, na kwa vile tuna uhitaji wa mabao mengi, tumeamua kuileta huku.

Pili ni wanachama na mashabiki wa Arusha hawajaiona timu yao ikicheza ‚laivu' kwa muda mrefu, mara ya mwisho ilikuwa ni Novemba, 2020 pale tulipocheza dhidi ya Coastal Union, sasa ni miaka minne imepita, mashabiki wa Simba Arusha wanaishia kuiona kwenye televisheni, tumeona wacha tuwapelekee na wao waende wakaione, na hiyo ni sababu ya kwanza iliyotufanya tuilete huku," alisema Ahmed.

Katika ushindi wa 7-0, mechi iliyochezwa Novemba 21, 2020 straika, John Bocco alifunga hat-trick, mabao mawili yakifungwa na Clatous Chama huku Hassan Dilunga na Benard Morrison wakifunga bao moja kila mmoja.

„Nyote mnafahamu tupo katika vita kubwa ya kuwania tiketi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao, nyote mnafahamu zilizosalia ni mechi za maamuzi na ngumu, hivyo lazima uzipeleke kwa watu wagumu ambao wanaweza kufanya mambo ili Simba kupata ushindi na watu wa aina hii wanapatikana Arusha," alisema Ahmed.



Wachezaji wa Yanga wakiwa pamoja na viongozi wao wakitambulishwa na Naibu Spika wa Bunge, Mussa Azzan ‚Zungu' walipofika kwa ajili ya kusikiliza hotuba ya bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ilipowasilishwa bungeni jijini, Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Azam yawaza dk. 180 Bara

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Azam FC, Youssouph Dabo, amesema mechi mbili zilizosalia za Ligi Kuu Tanzania Bara ni ‚muhimu mno' wachezaji wake kuonyesha ukomavu na kutumia vizuri kila nafasi itakayopatikana ili kujihakikishia wanavuna pointi sita.

Azam imebakiza mechi dhidi ya Kagera Sugar itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam itamaliza msimu ugenini kwa kuwafuata Geita Gold FC, mchezo utakaochezwa Mei 28, mwaka huu.

Dabo alisema ana kazi ya kuendelea kutengeneza mazingira mazuri ya wachezaji wake kuhakikisha hawapotezi nafasi ili kuondoka na ushindi wa idadi kubwa ya mabao na hatimaye kufikia malengo ya kucheza michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa msimu ujao.

Kocha huyo alisema Alisema mechi mbili ni muhimu kushinda na wachezaji wanatakiwa kuwa wakomavu na kutengeneza utulivu wanapokuwa na hata wasipokuwa na mpira ili kufikia malengo yao.

"Sio rahisi kushinda mechi, nimeongea na wachezaji wangu wanatakiwa wawe watulivu katika kila mchezo na kutumia vizuri nafasi zinazopatikana, ni muhimu kupata pointi tatu lakini kwa sasa kushinda idadi kubwa ya mabao ili tufikie malengo yetu," alisema Dabo.

Kocha huyo aliongeza wanahitaji umakini zaidi ili kuhakikisha hawapotezi alama hata moja kwa sababu wanajua wako katika vita ya kuwania nafasi ya pili.

# Aziz Ki atembea na mkataba wa Yanga

INATOKA UK. 24

Kiliongeza pia taarifa za nyota huyo kutakiwa na timu moja ya hapa nchini si kweli na hizo ni propaganda za usajili.

„Ofa ambayo Yanga wamempa si rahisi kwa Aziz Ki aiache, halafu asaini klabu ya hapa nchini, anachelewa kusaini kwa sababu ya ofa za nje ya nchi alizonazo, hakuna klabu ya ndani ambayo anaweza kwenda huko na kuacha ofa ya Yanga," kiliongeza.

Msemaji wa Yanga, Ali Kamwe, alikiri mchezaji huyo hajasaini mkataba mpya kwa sababu bado wapo katika mazungumzo.

„Niwatoe hofu mashabiki na wanachama wa Yanga, wachezaji wote ambao Yanga bado inawahitaji tutabaki nao msimu ujao, na hata kama kuna mchezaji ambaye tunamhitaji na akataka kuondoka hakuna timu ya hapa ndani inaweza kumchukua, labda ataenda nje ya nchi," alisema Kamwe.

Alitamba mwakani wanahitaji pia kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu na kufanya vizuri zaidi katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

„Tunataka msimu ujao kuandaa tena gwaride la ubingwa, ili tufanye hivyo lazima tuendelee kuwa na kikosi bora, Yanga itabaki na kikosi imara na bora zaidi msimu ujao," Kamwe aliongeza.

# Uwanja mpya watengewa bilioni 55/-

INATOKA UK. 24

„Kuhusu mradi wa ujenzi wa Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya, katika mwaka 2024/25 umetengewa jumla ya Sh. bilioni 1.5," Waziri Ndumbaro alisema na kuongeza kuwa: „Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na kuendelea kuimarisha ujenzi wa chuo kwa kufanya ukarabati wa miundombinu mbalimbali ikiwamo madarasa mawili, ukarabati wa uwanja wa ndani, ununuzi wa samani za chuo katika hosteli mpya iliyojengwa vikiwamo vitanda, magodoro na kabati pamoja na vitendea kazi vya chuo vinavyohusisha kompyuta na vifaa vya michezo."

Pia alisema mradi wa ujenzi wa Akademia ya Michezo Malya kwa mwaka 2024/25 umetengewa Sh. bilioni 10.2 kujenga miundombinu 193 vikiwamo viwanja vya mpira wa miguu, netiboli, kikapu, mikono, madarasa, bwalo la chakula, jengo la utawala na hosteli.

SIMBA, YANGA

Daktari huyo wa sheria alisema watashirikiana na wadau wengine kuhakikisha Ligi Kuu Tanzania, hususan michezo za watani wa jadi, Simba na Yanga, inakuwa na thamani kubwa, timu zinatengeneza uchumi na zinafanikiwa kufika zaidi ya robo fainali katika mashindano ya kimataifa.

„Tutahakikisha tunaondoa migogoro kwa wadau wa utamaduni, sanaa na michezo kwa kuwa na katiba mfano kwa vyama na mashirikisho yote itakayotumiwa na wote ili kuboresha usimamizi katika utekelezaji majukumu kwa vyama na mashirikisho ya utamaduni, sanaa na michezo nchini," alisema.

Waziri huyo alisema watatunga kanuni za uwazi katika matumizi ya fedha kwa vyama na mashirikisho ya michezo, pia kutunga na kuhuisha sera, mikakati, sheria, miongozo na kanuni za usimamizi wa sekta za utamaduni, sanaa na michezo ili kuzifanya zijiendeshe kibiashara zaidi, kuzalisha ajira na kujenga uchumi.

Alisema serikali itaendelea kuwezesha na kuzigharamia timu 10 za taifa kushiriki mashindano mbalimbali ya kimataifa.

Ili kutekeleza mikakati hiyo, Waziri Ndumbaro aliomba Bunge kuidhinisha Sh. bilioni 285.318 kwa ajili ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara kwa mwaka ujao wa fedha.

Michezo
Ijumaa Mei 24, 2024
Nipashe

## Kompany anukia Bayern Munich



UKURASA 21

# Uwanja mpya watengewa bilioni 55/-

### Mechi za 'dabi', Simba na Yanga zawekewa mkakati...



Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Dk. Damas Ndumbaro, akiwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025 Bungeni jijini, Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

**Na Faustine Feliciane**

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 55.5 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa uwanja mpya wa mpira wa miguu jijini Dodoma utakaokuwa na uwezo wa kuchukua watazamaji 30,000.

Idadi hiyo ya watazamaji ni sawa na ya Uwanja wa Samia unaojengwa jijini Arusha kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 112 (Sh. bilioni 286).

Kutengwa fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa uwanja wa kisasa jijini Dodoma kulitangazwa jana na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Damas Ndumbalo alipowasilisha bungeni makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha.

Alisema uwanja huo unajengwa katika eneo changamani la michezo Dodoma kama ilivyo kwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Alitaja shughuli zitakazotekelezwa katika ujenzi wa uwanja huo wa Dodoma ni pamoja na kuanza ujenzi wa kiwanja cha mpira wa miguu.

Ndumbaro alisema uwanja huo utajumuisha miundombinu ya uwanja wa ndani (indoor stadium), viwanja vya mpira wa mikono, pete na netiboli.

„Huu ni utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Mwaka 2020 hadi 2025," Ndumbaro alisema na kueleza kuwa serikali pia inaendelea na ujenzi wa Uwanja mpya wa Samia, jijini Arusha, ikitenga Sh. bilioni 125.3 kwa mwaka ujao wa fedha.

Alisema serikali inatekeleza miradi hiyo ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya michuano ya Mataifa ya Afrika (AFCON) 2027 ambayo Tanzania ni mwenyeji ikishirikiana na majirani Kenya na Uganda.

Mchakato wa ujenzi wa uwanja wa kisasa Dodoma ulianza wakati wa uongozi wa Rais John Magufuli, aliyeahidi kwamba Mfalme wa Morocco angetoa fedha kwa ajili ya mradi huo, lakini sasa serikali imeamua yenyewe kuutekeleza.

WASANII

Katika hotuba yake, Ndumbaro pia alisema Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania katika mwaka 2024/25 umepangiwa Sh. bilioni tatu ambazo zitatumika kutoa ruzuku na mikopo kwa wasanii nchini.

Alisema serikali pia itaendelea kutafuta fedha kutoka kwa wadau kwa ajili ya kuongeza mtaji ili wasanii wengi waweze kunufaika na kuwajengea uwezo ili kurasimisha kazi zao pamoja na kuziendeleza kibiashara.

INAENDELEA UK. 23

# Aziz Ki atembea na mkataba wa Yanga

**Na Faustine Feliciane**

UONGOZI wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, umesema unapambana kumshawishi mshambuliaji wake nyota, Stephanie Aziz Ki, ili asaini mkataba mpya wa kuendelea kuitumikia timu hiyo, imefahamika.

Taarifa zilizopatikana jijini, Dar es Salaam zinasema Yanga imefanya mazungumzo na nyota huyo lakini ameshindwa kukubali kusaini mkataba mpya kutokana na ofa mbalimbali alizonazo.

Chanzo hicho kimesema mchezaji huyo raia wa Burkina Faso anasubiri kufanya uamuzi mwingine baada ya kumalizika kwa msimu huu.




„Aziz Ki akiwa na wakala wake (mama yake), wamefanya mazungumzo vizuri na Yanga, lakini akawaambia wasubiri, atasaini siku nyingine, aliondoka na mkataba huo na kuahidi atausaini," kilisema chanzo chetu.

Kiliongeza licha ya Rais wa Yanga, Hersi Said, kuongoza kikao cha mazungumzo, Aziz Ki, alionekana kushikilia uamuzi wake wa kuhitaji muda ili kukamilisha mchakato huo.

„Uongozi tayari umempa mkataba mpya, lakini bado hajausaini, Aziz Ki anaonekana kuvutiwa zaidi na ofa kutoka Afrika Kusini kwa sababu kuna timu inamtaka, kuna uwezekano akaondoka," kilisema chanzo chetu.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >